# (CKRC)

# VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MATUGA CONSTITUENCY, HELD AT SHIMBA HILLS SECONDARY SCHOOL

ON

2ND MAY 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MATUGA CONSTITUENCY HELD AT SHIMBA HILLS SECONDAY SCHOOL ON 2ND MAY 2002**

**Present**

1. Dr. Mohammed Swazuri – Chairperson
2. Bishop B.K Njoroge – Commissioner
3. Nancy Baraza – Commissioner

**Secretariat Staff In Attendance**

1. Peter Apamo – Programme Officer
2. Edgar Kagoni – Assistant Programme Officer
3. Jacqueline Nyumoo – Verbatim Recorder

The meeting was called to order by Com. Swazuri and started at 10.00 a.m.

**Com. Swazuri:** Tuko tayari kuanza na tutaanza na maombi kutoka kwa Mzee Muthengi.

**Prayers by Mr. Muthengi**

**Mr. Muthengi:** Mungu baba wetu wa mbinguni, tuko mbele yako asubuhi ya leo. Tunatoa shukrani kwa ajili ya uwezo huu ambao umetupatia. Umetuamsha kila mtu mahali pake na umewalinda wageni ambao wamekuja na umewaleta salama na wamefika. Tunatoa shukrani zetu. Tunauweka mkutano mbele yako, tunaomba mwongozo wako ili ukaweze kutuongoza na ukaongoze viongozi ambao wanatuongoza ili waweze kutuongoza, na tukimaliza katika uongozi wako tutatoa shukrani. Tunaomba hayo tukiamini umetusikia kwa jina la Yesu Kristo Mkombozi wetu. Amen.

**Com. Swazuri:** Haya, wananchi watukufu kwanza tunataka kuwafahamisha wale Commissioners tulioko hapa. Niko na Bi.

Nancy Baraza, huyo ni Ccommissioner mama. Niko na Bishop Kariuki, huyo ni Commissioner na mimi naitwa Mohammed Swazuri ni commissioner. Kwa hivyo taratibu yetu ni kwamba kuna kutoa maoni mara tatu. Kuna kutoa maoni kwa mdomo pekee yake, tutakupa dakika tano, isizidi dakika tano ili kuwapatia watu wote nafasi. Kuna kutoa maoni kwa memorandum (mswada ulioandikwa) halafu mtu aupitie, atupatie yale mapendekezo sio kusoma huo mswada wote. Hata huyo mtu tutampatia dakika tano. Halafu kuna kutoa maoni kwa kutoa mswada pekee yake bila ya kuzungumza. Uje tu na memorandum yako na hutaki kuizungumzia sisi tutaenda kuisoma, hiyo utaitoa pale itarekodiwa pale. Na kila mwenye kuja kutoa maoni lazima kwanza aseme jina lake kwa sababu tuna-record halafu akimaliza kutoa maoni yake aende pale aandikishwe jina lake na kila kitu. Ni hapo au ni hapa? Ni hapo ee? Haya. Okey kwa hivyo tunaanza kwa sababu wananchi tunajua watakuja wengi. Tunaanza na mama, na leo ni siku nzuri tunaanza na mama. Serah Mumbi Mutuku. Ni memorandum utaisoma au, na upatie just recommendations. Haya, kaa pale.

**Serah Mutuku:** Asante sana kwa wakati huu. Jina langu ni Serah Mumbi Mutuku, mimi ni civic education provider wa Mangawani location. Maoni haya ambayo nitagusia ni kuhusu kina mama wa Mangawani. Nayo ni haya.

Namba moja, bwana akifa na mama awe na haki ya kupata uridhi wa bwana. Namba ya pili, bwana akimwacha mkewe awe haki na mali zigawanywe sawa sawa  baina yao wote wawili. Bwana awalee watoto wake wakiwa mikononi mwa mama yao hadi miaka kumi na minane. Namba nne, watoto wa kiume na wa kike wapewe elimu iliyo sawasawa. Watoto walio chini ya miaka kumi na nane wasilazimishwe kuolewa na mzazi atakayefanya hivyo achukuliwe hatua kali. Msichana ambaye amezaa mtoto na amtupe achukuliwe hatua kali sana na serikali. Watoto ambao wanatoa mimba wachukuliwe hatua kali sana na serikali. Mengine zaidi ya hayo, kile kitabu chekundu kile tulipewa juzi, tumejaribu kukipitia chote, tume-summarize, na ni yale ambayo nimepeana kule. Ni mengi singeweza kutoa maana hizo dakika tano ndizo nilizopewa. Asanteni sana.

**Com. Swazuri:** Asante sana mama umetuanzishia vizuri. Sasa tutamsikiliza mzee Johnson Muoka. Johnson Muoka yuko ama ametoka? Hajafika, kwa hivyo akija utatwambia uandike pale. Tuko na Philip Kamau, ndiye huyo. Mko pamoja okey.

**Mr. Willy Mutua:** Mimi ni Willy Mutua. Ni asante kwa kupata sulwa nimeelekea ya pili. Kuna kisemo ambayo nimekuwa nimebakisha hapa cha wanyama. Mimi nataka kama ng'ombe yangu inauawa na simba, hiyo ng'ombe tulipwe elfu thelathini, kama ng'ombe yangu imeshauawa na simba au ndovu. Kwanza mimi ningelipenda niseme hivi sisi mimi naona mambo mabaya au naona makosa makubwa sana kwa ufisadi. Serikali ni nzuri kutoka wakati tulipopata uhuru wetu. Ma-officers wanaofanya kazi kichakani, wanaofanya kazi kule mipakani, wanafanya kazi nzuri sana lakini kuna sababu moja ambayo ningelipenda irekebishwe. Kunapatikana mtu kule amefanya maajabu, ameua ama amefanya kitu kingine kibaya sana, amekamatwa lakini wakati atakapofungwa kutatokea mkubwa fulani na atamtembelea kule jela na hali kadhalika muda sio muda yule bwana anaonekana yuko nje. Ni ajabu sana ningelipendelea sana mtu kama yule akiwa yeye alifanya ni achukuliwa kabisa kabisa kulingana na vile alifanya.

Maoni ile ingine ningelipenda nitoe ni kuhusu wasichana ambao hapo awali zamani kulikuwa mtu akimdunga msichana mimba alikuwa akilisha yule mtoto miaka kumi na nane na siku hizi hakuna kitu kama hiyo. Kwa hivyo sina mengine ni hayo mawili. Hawa wasichana ningelipendelea irudi ile ile iliyokuwa zamani wakati tulipata uhuru. Kulikuwa wasichana wale yule bwana aliyemdunga mimba alishe yule mtoto mpaka afike miaka kumi na nane halafu kisha akitaka kumwoa amwoe. Thank you.

**Com. Swazuri:** Mwingine ni Daniel Mutinda Kyule.

**Daniel Mutinda Kyule:** Jina langu ni Daniel Mutinda Kyule na nina maoni yangu ambayo nataka Tume hii ya katiba iyarekebishe. Kwanza, naomba idara ya KWS ambayo iko karibu na sisi wananchi, pesa ambazo zinatolewa na watalii kutoka ng'ambo ziwe zikiwekwa katika wilaya yetu kwa maendeleo yake. Namba pili, kiwanda cha Ramisi cha sukari kifunguliwe tena ili mkulima wa Kwale awe kama yule wa Mumias na Muhoroni. Haya, namba tatu, moto ambao uko kama kilometer tisa kutoka hapa kutoka Mwavungo, ukiwa karibu na sisi wakulima wa Shimba Hills matunda yetu kama maembe machungwa na passion fruits yatakuwa na soko na kuhifadhiwa vizuri.

Namba nne, katika wizara ya wilaya, naomba pesa ambazo zinatolewa ushuru ziwe zikifanya kazi kama kutengeneza mabarabara zetu katika wilaya yetu. Namba tano, katika elimu, naomba angaa kuwe na cheo kidogo ili wilaya ionekane kama zile wilaya zingine katika kenya. Namba sita, katika mimea yetu, kuna mti kama mnazi na mti huu ndio una faida kuliko mimea mingine hapa Pwani. Kwa hivyo naomba maji yake yafanyiwe utafiti ili mkulima awe akiuza maji yake.

Uchaguzi wa viti- kuanzia mzee wa mtaa uwe wa mlolongo, chief, assistant chief, MP councillor na nominated MP hata rais na vipindi vya miaka, councilor miaka miwili, MP miaka mitatu, rais miaka minne. Utawala wa mkoa, tuwe na waziri mkuu. Raslimali yetu iwe ikitumika katika mkoa wetu. Asante.

**Com. Swazuri:** I think let us have the microphone there, I can speak loudly.

**Mr. Makau:** Nina yangu ambayo nitasema kidogo, memorandum itakuja baadaye. Kwa jina ni Phillip Makau Kamau. Nina maoni yangu machache ambayo ningependa ikiwezekana yachukuliwe. Natumaini ya kwanza nilikuwa nimeandika kiingereza ama itakuwa. Hii ni kuhusu mambo ya wanyama wa msitu na nimesema namna hii: any person attacked by wild animals outside the game reserve should be compensated. If one dies due to injuries got from wild animals should be paid one million Kenya shillings. If one has received injuries he should be compensated as per doctor's assessment. The government should be responsible for roads construction and repairs. If the roads are broken and the government takes long to repair the community should be empowered to accuse the government in a court of law.

Tatu, na hii nitasema kwa Kiswahili. Watoto wa kike wawe na haki ya kurithi mali ya wazazi wao kama vile shamba, nyumba, pesa na kadhalika. Nne, mke au bwana aliyeoa au kuolewa kisheria awe na haki kamili ya kurithi mali ya mumewe au mkewe. Tano, raia wa Kenya awe na haki kamili ya kumiliki ardhi mahali popote nchini Kenya mradi awe ameipata ardhi hiyo kisheria.

Asante.

**Com. Swazuri:** Sign kitabu chetu na uache memorandum hapo. Tutakuwa na Joseph M. Nguli.

**Mr. Nguli:** Makamishna mliotujia, ninayo maoni machache tu na nitazungumzia kuhusu ofisi ya makamu wa rais katika nchi. Kwa wakati huu tunajua ya kwamba makamu wa rais anachaguliwa na rais na inaonekana mara nyingi kuna shida ambayo hutokea anapotaka kutolewa. Makamu wa rais ninaonelea akichaguliwa na rais kama inavyofanyika, na adhibitishwe na bunge na akidhibitishwa na bunge aingie katika ofisi. Ofisi ya rais kwa wakati huu inaonekana ni kama haina wajibu ama nafasi yake ya kufanya, inategemea vile anavyopatiwa na rais. Ninaonelea kwa wakati huu katiba inayoandikwa, ofisi ya makamu wa rais iwe na uwezo, yaani iwe na wajibu ambayo anatimiza bila kupangiwa na rais na awe anafanya kazi bila kubadilishwa kama inavyofanyika wakati huu ili aweze kuwa na uwezo wa namna hiyo.

Maoni mengine ambayo ninatoa ni kuhusu wananchi wa Kenya. Wananchi wa Kenya, kama mwananchi yale ambaye ni mtu anayekuja akiwa ameamua kuwa raia wa Kenya, awe ni raia na bila kuwa na uraia wa nchi nyingine ili aweze kuwa raia mwaminifu katika nchi. Yale maoni mengine ambayo ninatoa ni kuhusu umilikaji wa mali katika nchi. Mwanakenya akiwa mahali popote katika Kenya aweze kutambulika. Kile anachokifanya, ikiwa ni anafanya kazi, yaani mfanyi kazi wa serikali, aweze kufanya kazi mahali pote katika nchi bila kulingana. Ikiwa ni mwalimu aweze kufanya kazi katika Nyanza, Coast, Eastern, kila mahali awe anaweza kufanya kazi na kulingana na uwezo wake. Maana inaonekana kuna udhaifu ulioko katika wakati huu ikiwa tunaweza kuwa tunahitaji waalimu wa kusomesha na waalimu tulio nao wanapandishwa vyeo kwa sababu ni wale ambao walio katika sehemu yao ya kuzaliwa.

Elimu haitakuwa sawa. Itaendelea kuwa kukiwa na tofauti maana ikiwa elimu wanaongoza, hawana uwezo wa kuimarisha ama kuinua elimu ni heri mchanganyiko ufanyike, mwalimu aweze kutoka North Eastern aje kufundisha katika Coast, mwalimu atoke katika Nyanza aende akafundishe Eastern ili tuweze kuwa na usawa katika nchi na elimu iweze kuwa sawa. Kwa hayo machache, asante.

**Com. Swazuri:** Asante. Bakari Dolla.

**Mr. Bakari:** Mimi jina langu naitwa Bakari Salim Dolla kutoka Mwapala minazini. Mimi yangu ni maoni na maoni yangu ya kwanza naonelea kwamba katika kila kijiji katika hapa kwetu kiwe na ulinzi wa kibinafsi kwanza mbali na kutegemea polisi au askari na kusudi ya kusema hivyo kwa sababu kuna ile inaitwa kamati ya ulinzi iwe dhabiti katika kila kijiji. Sio tu kamati ya ulinzi ya wangoje kumefanyika jambo halafu ndio waje wakae waseme labda ni fulani. Hiyo nilikuwa nataka iangaliwe sana.

Na oni la pili kwa mfano kuwe kumefanyika jambo katika kijiji halafu hatua ya kwanza ya kuchukuliwa inasemekana kwamba ni barobaro au vijana maanake sijui wanavuta bhangi sijui nini wanakuja kukusanywa na kuadhibiwa na ambapo vijana huwa

wako mara mbili kuna vijana wabaya na kuna vijana wazuri. Sasa ikiwa watachanganywa tu na kuadhibiwa kabla ya kuangaliwa mimi singeonelea iwe hivyo kwa sababu kama ni wazee pia wako wazuri na wabaya.

Jambo la tatu ni kwamba kuna nguo ambazo zimeshonwa kama za kuigiza askari au jeshi ambazo zinauzwa madukani mpaka sasa. Mtu anakwenda kununua nguo zile na anapawa risiti na punde si punde anaonekana nazo ananyanyaswa ama anaadhibiwa kwa kuambiwa: wewe ni askari? Kwa nini unavaa nguo ya askari? Na ninavyojua nguo ya askari haiwezi kuvaliwa na raia. Kwa hivyo mimi sitazungumza mengi, yangu ni hayo machache asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante sana Mzee Bakari. Tuko na mama Beatrice Mwamzuka.

**Mrs. Mwamzuka:** Ninashukuru. Mimi jina langu naitwa Beatrice Mwamzuka kutoka kijiji cha Mwanamkuu. Nazungumzia juu ya maoni ya Mpango Women Group. Na pia kwa niaba ya wanawake wa Mwaluvanga location pia nitazungumzia. Katika maoni yetu sisi wanampango women group tunapendelea ya kwamba ama tumeonelea kwamba jambo la kwanza kabisa huu uwezo uliopewa rais ni mkubwa zaidi sababu tukiangalia katika nguzo zetu za Kenya ni tatu. Tunayo nguzo ya serikali kuu, na ya mahakama, na ya siasa. Basi ingekuwa ni vizuri zaidi kama rais angesimamia nguzo moja na hii nguzo ya kama vile kuteua jaji mkuu au mawaziri au watu wengine wale wakubwa wakubwa hiyo iwe inasimamiwa na mkubwa mwingine mbali na rais. Hiyo ni sehemu ya kwanza. Sehemu ya pili katika rais, maoni yetu sisi wanampango tunasema ya kwamba, rais asiwe mbunge kama yeye anataka kugombea urais. Awe rais pekee yake, lakini mbunge hiyo sehemu ya ubunge, kama vile tunavyosikia huwa rais mpaka awe mbunge kwanza sehemu ya kwao, huo ubunge amwachie mwanakenya mwingine katika sehemu hiyo. Yeye asimamie urais pekee yake. Hilo ni jambo lingine.

Jambo jingine ni juu ya wanawake. Wanawake ni kwamba nao wapate viti sawa sawa na wanaume kama sehemu za ubunge. Basi na iendapo wameshindwa na kutosha wengi wa kutosha pengine, kuwe na utaratibu maalum hata kama ni interview wale wanaweza ku-qualify kwa masomo yao waongezewe, lakini waweze kuwa wengi ili kwamba waweze kupata nafasi ya kutetea haki za wanawake.

Sehemu nyingine ni kwamba tunao wazee wengine walafi ambao hurudia watoto wao kuwanajisi. Basi wazee kama hao, sisi tungependelea kwamba mzee akimnajisi mtoto mdogo au kuwanajisi watoto kwa ufupi, serikali iwachukulie hatua ya kutosha. Yule ambaye atakuwa amemnajisi mtoto mwingine aidha pengine apate adhabu za kama kufungwa miaka thelathini, au kama ni mzee ambaye amemnajisi mtoto wake aliyemzaa awe na adhabu mbali tofauti na ile ya yule mwingine. Hilo ni jambo lingine.

Jambo lingine nimesema nazungumzia kwa niaba ya makundi mawili, Mwaluvanga location na Mpango Women Group. Jambo lingine ni kwamba katika pesa zile huwa zilikuwa zikikaa kwa county council za wilaya, zilipopelekwa katika serikali kuu imekuwa ni matatizo makubwa kwa sababu zinapotoka kule ili kutengewa katika wilaya, zinakuja zazama zama humo vichakani na imekuwa ya kwamba sasa ni shida katika wilaya, na ndio sababu unaona barabara zingine kama huku ambako mali yote

yatoka huku mashambani, sisi tumekuwa watu wa kuteseka na pesa hizo zinafaidi watu wachache wale walio karibu na serikali. Sisi tumekuwa tuko mbali na serikali. Maoni yetu basi, kama sisi wanawake wa Mwaluvanga location, tunaomba ya kwamba pesa zile zirudi kwa mabaraza yake ili kwamba kwenye county council za wilaya ili wawe wanaweza kujipangia wenyewe.

Jambo lingine ni kwamba kuna hii soko inaitwa ya COMESA. Hii soko inaitwa ya COMESA, sisi hatukujua hiyo soko ya COMESA imetoka wapi, tulifanya kusikia kuna COMESA kukasemekana ya kwamba watu wana umoja lakini hata hivyo Mtanzania anapokuja hapa kuuza vitu vyake kama sokoni, yeye pesa za Kenya zinamfaidi lakini sisi pesa za Tanzania hazitufai. Hiyo pia nayo ni jambo lingine sisi wanawake wa Mwaluvanga location tumeona ni jambo limezidi kutuzorotesha katika hali ya uchumi wetu.

Jambo lingine ni juu ya elimu. Elimu imekuwa sasa wale ambao wanasoma ni wale watoto wa matajiri na wale ambao hawana kitu hawawezi kupata elimu kwa sababu zimeambiwa ni za bure lakini ni bure hakuna cha bure. Ni kwamba vitu vingi mzazi ndiye anagharimika. Kwa ufupi nitaacha hapo hiyo.

Jambo lingine ni juu ya afya ama hospitali.

**Com. Swazuri:** Unataka elimu iwe ya bure?

**Mrs. Mwamzuka:** Nataka elimu iwe ya bure ya kila kitu. Tusiambiwe ni ya bure halafu inaambiwa sijui mzazi afanye nini. Irudi kama pale mwanzo kwamba elimu ya msingi mpaka darasa la nane iwe ya bure ya kila kitu.

Mambo ya hospitali, tunapoangalia unajua unakuta ya kwamba maskini hata akiwa mgonjwa anaweza kufa kama katoto ka mbwa. Kwa sababu gani? Kwa sababu sasa hospitali zimekuwa ni pesa hazijulikani za private au hazijulikani ni za serikali. Imekuwa ni pesa kila mahali unapoenda ni pesa. Basi tajiri ndio ambaye hata akishikwa na ugonjwa gani, yeye yuapona. Maskini wanakufa kana kwamba si binadamu.

Jambo lingine ni juu ya raslimali. Tunaomba ya kwamba kila ukiwa unaridhi mahali uridhi juu mpaka mwisho na mpaka chini. Kumetokea msimu wa kwamba nikikutwa shamba langu linavitu ambavyo zinaweza kufaa, basi kunakuja watu wengine naambiwa napewa shillingi elfu thelathini ama hamsini niondoke hapo ili wapate kunufaika kwa ajili ya hiyo ardhi yangu. Asante kwa hayo machache na mengi asanteni.

**Com. Baraza:** Uliongea juu ya soko ya COMESA. Umesema, ninakuuliza swali. Umesema ya kwamba Watanzania wanakuja wanafaidika na pesa zetu na nyinyi hapa hamfaidiki na pesa za Tanzania. Hiyo ni kumaanisha ya kwamba pesa za Tanzania ni mbaya ama hamruhusiwi kwenda kuuza bidhaa zenu Tanzania?

**Mrs. Mwamzuka:** Pesa za Tanzania kama ni mbaya ama ni nzuri lakini ni ya kwamba sisi zikija hapa hazina nguvu kama zile zetu kule. Kwa hivyo kama ni usawa basi kama kunatakikana watu waungane, hizo za Tanzania pia sisi ziwe zinatufaa maana wakinunua kitu hapa shillingi kumi yeye anaenda kupata mia moja kule za Kenya anafaidika na za Kenya na sisi hatufaidiki na za Tanzania.

**Com. Baraza:** Lakini si mnaruhusiwa kwenda Tanzania kuuza bidhaa zenu?

**Mrs. Mwamzuka:** Sasa sisi hatujaenda na naona kama, sijui sana, lakini naona kama sisi haturuhusiwi kwa sababu sisi hatuchukui vitu vyetu kupeleka Tanzania, lakini Watanzania ndio wanakuja. Ijapokuwa hata kama tunaruhusiwa, tukiruhusiwa tukienda kule, bado zile pesa za kule hazitufai kwa sababu ukija nazo hapa hazina dhamani yoyote. Asante.

**Mr. James Ndambuki:** Kwa jina naitwa James Ndambuki. Waheshimiwa Makamishna, maoni yangu kwanza ni katiba inayoandikwa, iandikwe kwa lugha ya Kiswahili ili wananchi wengi waweze kujisomea. Jambo la pili ni ofisi ya rais. Ofisi ya rais imepewa mamlaka makubwa. Ipunguzwe mamlaka. Igawanywe. Rais awe kama chairman na asiwe na uwezo wa kuajiri watu. Kuwe kuna tume iliyoundwa ya kuangalia kila kitu. Rais pia hata akiwa Mkuu wa Majeshi asiwe na uwezo wa kuamuru majeshi yafanye kitu. Atakayeamuru majeshi yafanye kitu iwe ni bunge ndio itakayokuwa ikiongoza. Hata wale wabunge kumi na wawili wanaochaguliwa wabunge maalum wachaguliwe na tume, wasichaguliwe na mtu. Rais awe tu ni kama chairman wa kutia masahihi pekee yake mambo yakifanyika, lakini asiwe na uwezo wa kufanya kazi pekee yake. Pia kusiwe kuna mtu anayeangalia sheria pekee yake kuwa ni Mkuu wa Sheria pekee yake, hawezi kufanyiwa mashtaka akikosea.

Jambo la pili, ni kuhusu wafanyi kazi. Wafanyi kazi wanaoajiriwa na sheria ya miaka hamsini na tano wasifutwe kabla ya contract yao haijamalizika. Mtumishi ameajiriwa na sheria ya miaka hamsini na tano. Ikiwa haijamilizika asifutwe na mtu angojee mpaka kibali chake kile aliweka contractor kimalizike.

Jambo la tatu, ni kuhusu wanyama wa msituni. Wanyama wa msituni wamekuwa wakubwa sana kushinda binadamu kwa sababu wanakula mali ya mkulima na mkulima hana mtu mwingine aliyemwajiri, ameajiriwa na shamba, na hana mtu wa kumlipa ile mali yake ikiliwa na mnyama. Katiba ya leo iweze kumlinda mkulima ili mali yake ikiliwa na kitu chochote kilicholiwa na serikali alipwe haki yake.

Jambo la nne, ni kwamba mtu akiuawa na mnyama awe anaweza kulipwa shillingi milioni moja, ridhaa yake. Sio kama yale matusi yanafanywa unapatiwa shillingi elfu thelathini kama ya mazishi. Shillingi elfu thelathini ni kama ya mazishi. Shillingi elfu thelathini ni kama ya mazishi inayosemekana inalipwa mtu akiuawa. Hii ni katiba iliyo na makosa makubwa kumwonea mtu asiye na haki. Mtu aliye na haki aonewe na shillingi elfu thelathini badala ya shillingi millioni moja. Ikiwa yule mzazi alikuwa na watoto watabaki tu wakitangatanga wakichukua vitu mapipani.

Jambo la tano, ni kuhusu kina mama. Mabibi wanaolewa na sheria za kikabila ama za kikwao. Awe ana haki katika mali ya nyumba pahali alipoolewa. Ukikosana na bwana wagawanye mali usawa. Asiwe ni kama mtu alikuwa amekodishwa nyumba kukaa na mwenye nyumba baada ya kukosana anakufukuza anaenda bure. Kila mwanamke pahali anapokaa awe ana haki. Na pia kuhusu watoto, katiba ya Kenya iweze kuweka watu wa Kenya wote ikiwa mzee ana watoto kumi, wasichana watano na wavulana watano. Wakiwa wasichana hawakuolewa ile mali ya mzazi ikiwa itagawanywa wale waliobaki pale wagawanyiwe mali sawa na kila mtu kwa sababu wamezaliwa na mzee mmoja. Sio wazee wawili, ni mmoja na yule ni damu yake. Katiba ya kenya iweze kuweka hii kitu kwa njia ya sawasawa. Tunaona wanawake wengi ikiwa wasichana wamezaliwa sita na mvulana ni mmoja, wale wasichana mzee akifa, wanafukuzwa wote hapo nyumbani, yule kijana pekee yake anabaki na mali ya mzazi, anatawala pekee yake, na akina mama wanatangatanga kule wakiokota vitu wakitafuta watu kule njiani wa kuwasaidia na mali ya mzazi wao iko. Katiba ya Kenya iangalie usawa wa akina mama na watu waliozaliwa.

Jambo langu la mwisho, ni kuhusu wagonjwa. Siku hizi ugonjwa umekuwa na gharama kubwa sana na maskini hawaponi, wanakufa, kwa sababu hawana njia ya kutibiwa. Tungeuliza serikali ya Kenya iwe na njia ya kumwonea huruma mtu asiye na uwezo atibiwe ikiwa bado anaweza kutibiwa.

Jambo la mwisho ni kipande. Kipande tunachopata hapa Kenya, tukitaka kwenda nje, tupate passport kama kipande, bure bila gharama kwa sababu ni watoto wa Kenya, tuwe na haki hapa Kenya. Nikitoa ya mwisho nasema popote panakaa Mkenya ikiwa ni wapi awe ana haki kukaa pale bila ya kuingiliwa na mtu yeyote. Asanteni kwa hayo machache. Maoni yangu ndio hayo.

**Com. Swazuri:** Asante. Sasa tuko na Kalimbo Mtenzi.

**Mr. Kalimbo Mtenzi:** Mimi naitwa Kalimbo Mtenzi, Mnyawa, Jokore, kijiji cha Mauya. Basi maoni yangu kidogo nafikiri ni kama malalamiko ambayo inanihusu hapa Kenya. Nikifikiri na kuangalia mimi ni Mkenya na Kenya ni yetu na mwanakenya si haki alalamike. Squatter ni wengi Kwale. Sasa nataka mashamba wapewe wakenya wenyewe. Nikipata shamba sitaki ndovu mahali panapokaa binadamu asifike ndovu, afungiwe sehemu yake. Sababu hapa nimekuja mwaka wa sabini na sita. Kazi yangu ni kuomba shamba. Nipewe msitu, nikateke pale, niweke mwenyewe korosho yake, kila kitu nifukuzwe, niende pale, nifukuzwe. Hata hivi sina makao kama mwanakenya.

Mwanakenya awezaje kuteseka na Kenya yake? Hata aliye na kibali awe na mnyama msituni ambapo ndovu, nyani, nyati awe na makao lakini binadamu kama mimi nikose makao na ni mwanakenya. Niende wapi? Nikizungumza hivyo, vyombo vyangu vitaliwa na ndovu na mimi ni mwombaji, shamba sina. Nikizungumza kwa serikali mbona naambiwa ukae rafiki na ndovu wewe. Sasa ni mimi nilime ndovu aje ale, nakulipaje na shamba sina. Kizazi hiki kitakuwa namna gani maisha ya vijukuu na hakuna nafasi, hakuna nafasi ya shamba? Mimi nina wajukuu wangu na wanangu nitaishi namna gani, nataka shamba. Msitu uko tele.

Ndovu ametengewa sehemu yake lakini binadamu hafai kuliko mnyama. Hii ni kweli Mkenya ateseke na Kenya yake?

Naomba serikali kama inawezekana katiba hii nataka shamba, msitu uko tele umeteka Miritini mpaka Ribe karibu na Lungalunga, umetengewa wanyama. Mimi ninateseka, sina mahali. Nataka shamba msitu upasuliwe, wanyama watengewe sehemu yao na binadamu sehemu yao. Kila mtu aridhike na anufaike na matunda ya Kenya kama Kalimbo ninavyosema.

Lingine nataka Majimbo na utawala kwetu karibu na mwananchi. Nataka Majimbo na utawala uletwe karibu na mwananchi. Kitokacho hapa Pwani, kiliwe na mwenyewe. Watoto wetu, wakisoma hawaendi mbele kwa sababu hatuna vyuo vya ufundi. Twataka kila wilaya kujengwe vyuo vikuu. Katika sub-chief aondolewe maana hana kazi. Sub-chief kazi yake anayegandamiza chairman wa village. DC akitoa huko habari kuhusu DO, DO akimpa chifu, chifu anampa sub-chief, sub-chief anakaa anaita ma-chairman waeleze mikutano yeye anakaa tu. Hata DC akija watu wako tele anasema ndio kazi yangu imefanya vizuri. Yeye ameketi kazi ni ya ma-chairman, ma-chairman wanateseka mbaya sana na hapati kitu na halishwi kitu. Nataka chairman na chifu pekee yake wanaweza hiyo kazi, iwe sub-chief hana kazi.

**Com. Swazuri:** Sasa unataka chairman alipwe mshahara au?

**Mr. Kalimbo:** Hata asipolipwa mshahara lakini naona kama ni sawasawa kwa kazi yake hiyo na wale waliomkujilia pale kumshtakia hivyo itakuwa ni sawa. Kwa hivyo pekee yake hata mtu akisema anakuja kushtaki sababu chief anachukua jukumu kesi anaitengeza yeye chairman anakuwa sauti. Hapo sub-chief hana kazi. Lingine sina zaidi isipokuwa ni kama hilo sikitiko ya kwamba binadamu akiwa hana shamba ameuawa na kizazi chake hakiendi mahali popote. Sasa amekufa pamoja na vijukuu vyake. Nataka msitu upasuliwe huu. Binadamu kwao na ndovu kwao.

**Com. Swazuri:** Andika jina lako pale.

**Mr. Muoka:** Jina langu ni Johnson Muoka. Mimi nina maoni sio mengi ni kama matatu hivi. Maoni ya kwanza ni kuhusu distribution of national resources. Kwanza naona kugawanywa kwa huduma za serikali katika wilaya si sawa kwa sababu utakuta wilaya zingine. Zingine zina mabarabara mengi ya lami kushinda zingine hata hazina hata barabara moja ya lami. Pia huduma kama umeme katika sehemu za mashambani ni kama unatolewa kiubaguzi. Kuna sehemu zingine utakuta hata nyumba ya nyasi imetiwa umeme lakini kule ambako watu wanataka kuendelea umeme haupatikani. Kwa hivyo ningeomba katiba itakayoundwa ihakikishe ya kwamba serikali itagawa huduma zile muhimu kama umeme, barabara za lami na maji ziwe zinagawanywa kisawa kwa usawa katika development areas zote za district zote. Kusiwe area moja inawachwa inakuwa developed kuliko ile ingine. Hiyo ni namba moja.

Namba pili, ni kuhusu wakuu wa sheria na pia wakuu wa vikosi vya silaha. Ningependa baada ya kuteuliwa na kiongozi wa taifa wawe wana-vettiwa na parliament kuhakikisha ya kwamba hakuna mtu ambaye rekodi yake ni mbaya. Atachaguliwa kuwa

katibu mkuu au waziri au amiri jeshi au mkuu wa sheria au jaji mkuu wa mahakama. Hivyo vyeo ni vyeo muhimu katika serikali na ingekuwa bunge ina uwezo wa ku-vett angekuwa hakuna utatanishi au ufisadi mwingi katika zile afisi kubwa.

Pia, ilikuwa ni maoni yangu ya kwamba elimu ya msingi ifadhiliwe na serikali kutoka kidato cha kwanza mpaka cha nane. Pamoja na vitabu vyote na malipo ya waalimu isiwe mzazi anadaiwa chochote isipokuwa ile ya elimu ya shule ya upili, hapo mzazi anaweza kuanza kugharimika. Maoni yangu itafikia hapo asanteni.

**Com. Swazuri:** Benard Gichuki na nimekupa dakika tano.

**Mr. Gichuki:** Asante sana makamishna na wananchi watukufu. Yangu si mengi ila tu ningegusia kidogo kuhusu ofisi ya rais. Huku chini, grassroots, tuna mzee wa mtaa ambaye anafanya kazi kupita kiasi, na huyu bwana halipwi na anatakiwa ahesabu watu vijijini. Anatakiwa kwa kesi kama nyumbani, na hali akipokea haya yote anapeleka kwa sub-chief. Sub-chief, sijui anapelekea chief au DO hatujui. Huyu bwana anafanya kazi halipwi, anaacha kazi zake nyumbani akafanye kazi ya serikali. Inafaa alipwe. Awe na mshahara kama wengine. Turuke hapo. Chief, sub-chief wawe wakipata uhamisho kama vile DO, DC, PC wanapata uhamisho na ndipo wakienda nje watakusanya maoni vichwani vyao, watakuwa wakielewa jinsi ya kutawala. Kwa hivyo inafaa wapate uhamisho.

Nitaruka, upande wa wanyama wa pori tunaona mbuga nyingi za wanyama zimewekwa ua, fence. Mwananchi wa kawaida analazimishwa kulimia ile fence na wale ni ng’ombe wa mtu fulani ambaye wanamfaidi yeye na huku mwananchi anaambiwa wanyama ni wako na ila kuna mtu fulani ambaye anatumia wale wanyama. Mwananchi anaamka akalimie waya, halipwi. Inakuwa ni kama mtumwa. Kwa hivyo KWS ilime waya ni yao, ndovu ni wao, nyati ni wao sio wa mwananchi maana hafaidi. Faida ya mwananchi na wale wanyama ni mali yake shambani kuharibiwa na halipwi bado. Hiyo ndio faida ya mwananchi kweli? Tunataka KWS ilimie waya na ilinde wanyama wasirukie wananchi popote pale Kenya.

Tutoke hapo, mnyama anakuua wewe mwananchi. Ni ndovu, ni simba, ni nani. Ukiuawa ulipwe elfu thelathini. Ni kuku, ni mtu? Tunataka mwananchi au binadamu yeyote akiuawa na mnyama asilipwe chini ya milioni ishirini sababu mimi nina umri wa miaka ishirini, nimeuawa na ndovu, ningekuwa na billionaire mimi hapa nchini. Nitalipwaje shillingi thelathini elfu? Kwa hivyo mwananchi au binadamu alipwe akiuawa na mnyama.

Turuke hapo, tukiingia katika town kama coastal strip, utaona ya kwamba mimi nimeuziwa uwanja kama Mombasa, Ukunda, nijenge jumba langu kama hili. Bado, mimi ni squatter, nalipa mtu hiyo ardhi. Kwa nini asiniuzie hiyo ardhi na nipewe kibali cha kuwa ardhi ni yangu. Kwa hivyo tunataka ukiuziwa ardhi upewe title deed, ile ardhi iwe ni yako maana itakuwezesha kuchukua mkopo popote pale. Tunaomba tupewe jukumu. Ikiwa hiyo ardhi ni yako au shamba lako pale pia una shamba wamekuja watafuta madini, wakute kuna mafuta, kuna madini ya aina Fulani, itakuwa wewe ni mtu wa kufukuzwa au upewe elfu mbili tatu, ondoka hapa. Ndio wanao uwezo wachukue ile ardhi. Tunaomba katiba itakayoundwa hiyo ardhi kutoka juu na chini iwe ni

mali yako. Isiwe mali ya mtu. Nafikiri commissioners nitakoma hapo kidogo.

**Com. Baraza:** Hawa wanyama wa pori umesema wanatembea, ati mnatembea pamoja ama wako na….

**Mr. Gichuki:** Wako na vifaa kivyao na wanavunja ule uwa wanaingia kwa wananchi, wanaharibu mimea ya wananchi na wanaua wananchi.

**Com. Baraza:** Na tukisema sheria mpya iwalinde nyinyi ndio wanyama wasivuke mpaka, na nyinyi pia mpate income ya hiyo KWS, hiyo itakuwa sawa?

**Mr. Gichuki:** Kwa mfano ikiwa tutalindwa kama katiba ambayo inasema mwananchi alindwe na mali yake. Hii katiba mwananchi alindwe, mnyama na akae kwake.Wacha sisi binadamu tukae kwetu.

**Com. Swazuri:** Hassan Ali Mwang'ombe.

**Mr. Mwang'ombe:** Jina langu naitwa Hassan Ali Mwang'ombe, kwanza nawaamkua, Salaam Aleikum.

**Audience:** Aleikum Salaam.

**Mr. Mwang'ombe:** Na makamishna wote, hamjambo?

**Commissioners:** Hatujambo.

**Mr. Mwang'ombe:** Nawakaribisha nikiwaambia karibu sana hapa ni Shimba Hills. Mimi ni mdigo wa Shimba Hills. Nashukuru sana, yangu nikuwashukuru kwa kazi hizi mnazozifanya na kazi za amani. Mimi ndiye KANU youth wing wa area hii Kubo division. Langu ni ombi tu na kuwashukuru na kazi zenu. Shida ya Kubo hii hakuna vitu kadha wa kadha. Hakuna barabara, hakuna hospitali, hakuna mafanikio ya mashambani, hakuna mikopo. Area hii ni kama ambayo imetupwa, haina msimamizi ambayo area hii iliwapokea wananchi wenzetu tunawashukuru tunaishi nao sasa ni miaka arobaini hapa Shimba Hills, nikisema kwamba mimi ni mdigo.

Nawashukuru hawa wote walioko hapa kwa heshima zao na mambo yao, lakini serikali imewatupa hawa pamoja na sisi wenyewe. Hatuna njia ya kufanya. Kila tukipiga kelele hakuna kitu kinakuja hapa. Tunachagua bunge hakuna kitu, ma-councillors hakuna kitu. Fikira ni kitu gani hapa sasa waume? Fikira za hapa ni kufikiri kama Mungu atajalia watakuja watu watatusaidia. Nafikiri ndio nyinyi Mwenyezi Mungu awasaidie na baraka zenu karibuni ikiwa hapa ndio Kubo Division, Shimba Hills, Mwagozo, Mwaluvanga Location. Asante.

**Com. Swazuri:** Asante sana ujumbe tutaupeleka mzee ya kwamba kuwe na development kila mahali. Asante sana na uende pale uandike. Katana Katenga. Karibu Mzee. Utafuatiwa na Joseph Ndolo ajiweke tayari.

**Mr. Katana:** Asante sana wakubwa wa mkao huu. Mimi kwa majina naitwa Katana Katenga mkaaji wa Boyani Sub-location, Majimboni Location Shimba Hills, Kubo Division. Mimi sina maoni mengi sana maana ni mzee, fikira za wazee haziendi mbali sana. Kwa hivyo maoni yangu ya kwanza ninaomba serikali ikiwa inawezekana mwananchi apate maji kila mahali pale alipo. Tupate kujisaidia na kupitia mashambani mwetu yaani mtu kuna wakati mwingine kuna jua kali sana na tunapata shida kwa maji. Waweza kuteka kama hapa maili tano hivi kwa maji, visima vimekauka waenda kisima kile kimekauka, akina mama hukesha huko kwa maji. Mimi naomba ikiwa inawezekana katiba hii mpya itosheleze maji wananchi kila mahali alipo.

La pili naomba ikiwezekana, iwe ikifika mwezi wa pili kila mwaka, barabara zetu hizi ziwe zimesafishwa vizuri hatuna shida kusafirisha mali zetu kupeleka Mombasa. Tatu, maoni hii yangu ya kuomba, ninaomba mimi pale nitokapo Boyani Sub-location mimi ni mzee wa kijiji mdogo lakini tunapata shida. Tukiletewa barua kutoka kwa bwana chief na ma DO ikija kwa bwana assistant chief sasa anatutuma wazee wake. Tunatembea mguu mji kwa mji kutangaza mkutano. Ukifika pale mheshimiwa mwenye kumtangazia mkutano wake atakuta wananchi wa Boyani Sublocation wamejazana kweli kweli kwa sababu ya mzee wa mtaa, na hatuna tupatalo, ni kujitolea wenyewe tu tumechaguliwa na wananchi na kujitolea kupenda yaani kulinda usalama pamoja na serikali yetu ya Kenya.

Hatutaki mwananchi mahali alipo anyanyaswe. Na wakitatizana wenyewe kule wananchi wanakuja kwetu ofisini kwa assistant chief wetu kuja kutangaza kuwa sasa mimi nataka fulani aje amenifanyia mabaya sana. Amenifanya hivi na hivi, halafu anapata barua yule mtu anakuja, wazee sote tuko pale tunatatua yale maneno. Kwa hivyo ikiwa inawezekana wapate mshahara. Nishamaliza. Asanteni sana wakubwa nyote, Mungu ambariki.

**Com. Swazuri:** Andika jina lako pale. Tunataka Pastor Joseph Ndolo.

**Pastor Ndolo:** Asanteni sana commissioners na wahudhuriaji mliohudhuria kikao hichi kwa ajili ya kutoa maelekezo yenu. Mimi ni Pastor Joseph Ndolo, ni mkaaji wa hapa Shimba Hills na nina mapendekezo hata iwapo mengine yako tu katika katiba ile ninajua ya kwamba yatakuwa na nguvu kwa sababu ya katiba hii ambayo commissioners wako katika Kenya nzima wakitafuta mapendekezo ya wananchi wa Kenya. Nina points kama kumi na moja na nimeziandika kwa Kiingereza lakini nitajaribu tu ili wananchi wanisikie kubadilisha kwa Kiswahili.

Ile point ya kwanza iko Chapter 5 katika katiba Constitution of Kenya. Protection of fundamental rights and freedoms of the individual. Section 82, kwamba inasema kila mwanakenya anahitajika kuishi kwa amani. Mimi nami nasema kila mwanakenya ahitajika aishi kwa amani, aishi mahali popote Kenya, mradi tu awe anaendeleza taifa letu. Hiyo ni point ya kwanza.

Point ya pili iko Chapter 2, the executive, part one section 14 katika katiba ya mbele. Mimi ningependekeza kwamba hakuna mwana Kenya yoyote angeruhusiwa kuwa juu ya sheria, above the law, kwa sababu tunaona mtu akiwa juu ya sheria hana mahali popote pa kufanyiwa prosecution, mashtaka hawezi kufanyiwa na hii imesababisha nchi nyingi za Afrika kuwa katika matatizo kwa sababu ya kuangalia mtu mmoja ambaye yuko mtu mmoja ambaye yuko juu ya sheria na huyo anaweza kutenda kitendo chochote akijua kwamba atafanyiwa chochote. Kwa hivyo Kenya haihitaji kuwa na kiongozi au mtu yeyote atakayekuwa juu ya sheria.

Tatu, hii ni Chapter 7, habari ya government finance. Mara nyingi serikali inasomewa budget kila mwaka na tunaposikia ikisomwa mara nyingine hao parliamentarians wanatoka wakisema ni sawa na siku mbili wanasema sivyo. Basi ni mapendekezo yangu parliament, national assembly ipate kuangalia na kudhibitisha kwamba kile kinasomwa ni cha sawa. Serikali itakayokuja national assembly hiyo kamati iangalie, ichunguze kwamba budget ya mwaka inayosomwa inasomwa katika haki na wala si vitu ambavyo haviko.

Chapter 5 section 82 sub section 1 mpaka 9, inasema serikali itakayokuweko ipeleleze, itafute ni kwa nini katika mikoa miwili Rift Valley na Coast Province kulikuwa na tribal clashes tunapoelekea elections. Ichunguze, si kamati tena ambayo imeteuliwa. Serikali ichunguze ni kwa nini kumekuwa kila tunapoelekea uchaguzi vita baina ya makabila ya Kenya.

Namba tano, Chapter 2, hiyo ni executive. Section 5, rais wa nchi atakapochaguliwa awe ni mtu mature aliye na elimu isiyo chini ya degree, awe ni mtu anayekubalika katika taifa kwa yale aliyotendea taifa siku za nyuma kabla hajachukua hivyo. Namba 2, awe si Member of Parliament katika ile constituency yake.

Section 12 na kuendelea hapo, na (b) yake inasema rais aki-mess, akifanya makosa na ofisi, national assembly ichukue hatua mara moja asimamishwe na deputy wake ama makamu wake ashikilie ofisi maana kule kumwacha pale ataendelea ku-exploit the nation, ataendelea kuharibu taifa. Nataka kukazana tena ile ingine ni local government ambapo tuna local authority. Councilors watakaochaguliwa ni mapendekezo yangu miaka ijayo wawe councillor kama vile tumesema president awe ni mtu ambaye ana degree na above, basi councillor naye awe hayuko chini ya form four, awe amehitimu elimu ya form four.

Namba saba, basic rights. Watu ambao wanafanya kazi - civil servants, watumishi wa serikali - wasije wakastaafishwa kabla ya miaka yao kufika. Katiba iseme kwamba hakuna kustaafisha Mwanakenya kabla ya wakati wake maana ni kusababisha kuleta shida na hii ndio imeleta taabu nyingi, mambo ya wizi na uharibifu mkubwa, maana mtu amefanya kazi miaka miwili katika serikali na anasimamishwa na hana mahali popote pa kwenda, kuna lack of work, halafu sasa atachukua bunduki. Atainunua mahali atakapoipata aendelee kuharibu peace. Kwa hivyo retirement age iwe ni 55 kama kawaida. Mtu afanye kazi bila kusumbuliwa.

Land and property rights- Mwanakenya yeyote awe amepatiwa documents au kama title deed popote alipo. Awe na documents zinazom-support kwamba yuko Nakuru ama yuko Tana River lakini ni mkulima aliye na documents.

Succession and transfer of power…(naenda kumaliza). Vice president aendelee kushikilia ofisi ya rais wakati tunapotafuta ni nani atakayekuwa rais wa nchi.

Legislature - ni maoni yangu kwamba vyama vinavyotawala, vyama vilivyo katika serikali wakati wa ku-share ministries, wagawanye ministries wote kwa sababu ruling party ikiwa ni hiyo tu ndipo kunabaki sehemu zingine ambazo kile chama hakikupata majority, hatukupata watu wengi, inakuwa ignored. Ile sehemu inakuwa haijaliwi na kwa hivyo ruling party inaendelea ku-develop zile sehemu ambao wanajua kwamba wana watu wengi. Ni mapendekezo yangu watu wagawanye. Kama ni DP iwe ina-share some of ministries, kama ni… vile vyama viko vipate ku-share ministries ili development iwe shared equally.

Ile ya mwisho ninasema ni kwamba katika serikali kuwe kuna kamati iliyoteuliwa inayoangalia mishahara ya watumishi wote, civil servants, watumishi wote, kamati iliyoteuliwa ambayo inatoa mishahara ya wabunge, inatoa mishahara hata ya rais na mishahara ya watumishi wote wa serikali. Pia mtu ambaye amefanya kazi miaka mitatu awe anaweza kupata automatic promotion kama haja-mess na ofisi. Basi ninatumaini commissioners, hayo ndiyo mapendekezo yangu na pia kwa sababu nimeandika na lugha ya Kiingereza ningetaka kuwaachia kwa ile amendment. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Basi tumpate Willy Mutua.

**Mr. Mutua:** Mimi naitwa Willy Mutua, ni mkaaji wa hapa Shimba Hills headquater. Nina miaka arobaini na tatu hapa Shimba Hills tangu niingie hapa. Pendekezo yangu ni wanyama wa porini. Ndovu, nyati, na manyani. Hiyo ni kitu imesumbua mwananchi hapa Shimba Hills wakati nimeingia hapa. Watu tulishashuhudia wengi ambao wameshauawa hapa na ukisikia mwananchi ambaye amelipwa hicho ni kitu cha ajabu sana. Wanalipwa thelathini elfu tu. Hiyo si kazi ya binadamu hiyo. Mtu hawezi kulipwa pesa kama hiyo. Nataka alipwe milioni tatu kwa maana huyu ni mwananchi ambaye ameacha family yake, ameuawa, na hatapatikana maisha yake. Tunataka mwananchi huyu ahifadhiwe kwa maana sheria za nchi hii zinasema mwananchi atalindwa na mali yake. Na halindwi. Tumeshuhudia hapa, waya zile zinaambiwa ziwekwe moto hazina moto saa hii, na ndovu ameshaingia hapa. Ukiinuka asubuhi mwananchi yeyote ambaye ni mzalendo wa Kenya analala shambani kufikia saa kumi na mbili mpaka saa kumi na mbili, ili ndovu wao hawawezi kutoka hapa. Ukiinuka tu, ukiangalia tu unakutana na ndovu ndio huyu. Tunataka mwananchi alindwe. Sheria katiba inasema mwananchi atalindwa na mali yake na hatulindwi. Tumeshuhudia hapa ndovu ikizaa hapa makope sehemu fulani na tukawaita hapa wachukue ndovu amezaa na hakuchukuliwa.

Ingine ni tunataka tuletewe stima. Hapa sehemu hii haina stima kwa maana stima ni kitu muhimu sana. Hapa sisi ni watu ambao ni wakulima. Tuna wakulima. Tuna machungwa, tuna maembe na hiyo stima ikiletwa hapa itakuwa sisi tunafaidika. Itakuwa mali

yetu haiharibiki. Kwa hivyo tuletewe stima, na tukiletewa tusije tukalipishwa; stima ni ya bure.

Barabara:- barabara tumepata shida tangu wananchi waingie hapa Kubo Division. Unaweza kuangalia hapa kama vile unaona hapa, sehemu ambayo umekuja kusikia mwananchi. Barabara hakuna, shida kutoka hapa kwenda Mkongani. Hata ukiangalia wananchi hapa ni wabaya, na kuna sehemu ingine ambayo iko na ndovu. Tutengenezewe barabara kwa maana udanganyaji huu tunadanganywa hapa, mimi nimewahi kuhudhuria sub-DDC hapa na ndio. Lakini nimesikia officer wa rural akituhakikishia akiwa katika sub-DDC kutoka Mwavungo kwenda Kiemu tutapewa 1.4 million itengeneze barabara hii. Tukiangalia dakika hii haijatengenezwa. Mzalendo wa Kenya angali anapata taabu sana. Mawasiliano na magari hakuna kwa maana mwananchi yeyote hawezi kuleta gari yetu hapa. Hata wengine hawanunui gari hapa kwa maana hii ni sehemu ya kuteleza, ina milima, gari haiwezi kuingia. Kwa hivyo hiyo barabara tutengenezewe, na tukitengenezewa sisi wakulima hatuna maneno mengi. Sisi tunasema okey.

Hospitali:- hospitali ni kitu kinatusumbua. Malipo ya hospitali, mwananchi huyu, mzalendo huyu, hana pesa ya kwenda kugawanya ile gharama iko pale. Unaweza kukuta wengine kwa maana hana pesa, msimu ambao huwa uko hapa huwa ni msimu ambao saa ingine kuna chakula, saa ingine hakuna, kwa hivyo kugawana gharama pale hakuna. Tunataka sisi hospitali ijengwe na iwe ni ya bure. Hapana lipa pesa. Hospitali ni yetu, twende bure, na serikali ituletee ambulance kwa maana dakika hii tumeshuhudia watu wanakufa hapa kwa kukosa ambulance ya kuwabeba. Kwa sababu shida iko hapa, ukitoka hapa unaanza kubebwa na baiskeli, mama ni mgonjwa na ana mimba. Wengine nimeshuhudia wakifa njiani wakielekea Msambweni na huyu mama akapoteza maisha yake na mtoto akapoteza maisha yake.

Tunataka tujengewe hospitali, hospitali nzuri, sio hospitali hoi hoi. Tuwe na hospitali nzuri kwa maana sehemu hii ina wakaaji wengi sana. Wengi wameuawa na malaria kwa hivyo tuletewe madawa na tuletewe net. Watu wengi wameuawa na malaria, wakubwa na wadogo. Tupatiwe net na tuhifadhiwe kama wananchi wa Kenya hii. Thank you very much.

**Com. Baraza:** Bwana Willy, wewe unaelimisha watoto wako?

**Mr. Mutua:** Ndiyo.

**Com. Baraza:** Uko na fees?

**Mr. Mutua:** Fees tunalipa, lakini huwa ni shida sana kwa maana kama mimi sikuuza chochote na mimi ni mkulima wa kawaida huwa watoto wengi wako nyumbani. Hata saa hii shule… tunataka tusaidiwe ni serikali kwa fees. Hatujui kama wengine watakuja shule kwa ajili ya matatizo ya fees. Hiyo tuangaliliwe na serikali.

**Com. Swazuri:** Tumpate Francis Kianga.

**Mr. Kianga:** Mimi, kwa jina ni Francis Kianga, secretary wa Farmers Association, Kubo. Nina memorandum hapa nitapitia through in summary ambayo nitaomba muweze kuchukua. Utangulizi( Preamble) – We the people of the Republic of Kenya, all sovereignity and powers belong to us. We recognize our struggle against injustice discrimination and corruption. We endeavour to promote ethical public standards, justice and freedom for all of us. Huo ni utangulizi.

The new constitution should uphold the will of the people of kenya above all government institutions. No sector of our society should be marginalized. Kenya should have a coalition government of national unity where all the parties have proportionally represented. About land- there is severe landlessness in our country while large masses of land lie idle in the name of forests and game reserves. In reality the people around the game reserve do not benefit instead the animals loiter and kill people and devastate their farms. A part of the land should be set apart to settle the landless around the forest. Land shares certificates and title deeds should be issued to every land owner.

The farmer himself - the Kenyan farmer, especially the Bixa Anato farmer, mkulima wa Biksa katika area hii, has suffered because of a very bad legislation. The legislation that requires one to obtain an export licence inorder to market farm produce abroad should be repealed. And again, the Agriculture Act Cap. 318 of Laws of Kenya Part 15 of the development of certain crops, Section 190,191 and more particularly 192(1)(8)(7) which reads inter alia: to regulate and control the marketing of crops by growers and other including the requiring of the growers and other to sell crops to a particular person only. This legislation is not in line with the international and currently the government policy of liberalization and is against the implementation of Structural Adjustment Programmes.

The legislation grants direct monopoly to one company - the Kenya Bixa- around here. Therefore the farmer should be left alone to handle and market their produce without interference from the government, that is Part 15 Section 190 and 191,192,(1h),(7) should be repealed. Sheria hiyo iondolewe maanake inagandamiza mwananchi wa hapa na watoto hawawezi kusoma kwa sababu anategemea rangi na watoto wa hapa hawasomi kwa sababu mkulima wa hapa anategemea rangi na hakuna mahali anaweza kuuza mahali popote. Imekuwa monopoly imerudishwa Kenya ambapo ilikuwa imeondolewa.

The government itself. The three instruments of the government, the executive and the legislature and the judiciary should be independent from each other. Bunge, mahakama na utawala, sehemu hizo zisihusiane kuhudumiana. Utawala wenyewe - there should be a president who should be elected by the people to run for two terms of five years each. There should be a Prime Minister and a deputy Prime Minister who should be elected by the people after every five years. The president's personal and official conduct must be subject to the same laws that apply to any other Kenyan citizen. Lazima rais katika katiba mpya awe anaweza kuhukumiwa na sheria yoyote ile inahukumu mwananchi yeyote hapa Kenya.

Baada ya kifo cha president, the Speaker of the National Assembly or the Chief Justice should have the power to act as the President. The Speaker of the National Assembly or the Chief Justice. Either of them should have the power to act as the president for any period after the death of or the resignation of the president for the period as will be decided by the parliament. Section 25, (1) of the current constitution should be repealed so as to remove the president's absolute power of appointing and dismissing civil servants. Hiyo sehemu iondolewe katika katiba kabisa. Rais hawezi kuajiri na kufuta watu wakati anapenda.

The appointments of the senior officers of other constitutional offices must require total consultation of public and other civil societies but this one must be vetted by the committee of the parliament. And this committee must be chaired by an opposition party. Legislature. (Will you allow me to read the last one? Thank you, I will hand over to you). The new constitution should allow for devolution of power. Power should be decentralized and should ensure that there are checks and balances within the government institutions to the local authorities.

**Mr. Wambua:** Asante sana Commissioners na wananchi kwa jumla. Mimi naitwa Joseph Wambua Kaseng'a. Mimi ni mkaaji wa sehemu ambayo inaitwa Kidongo, iko katika Makope sub-location, Majimboni location, Kubo Division. Mimi sina mengi kwa sababu yale ambayo nilikuwa nimeyapanga yamezungumzwa na wengi lakini sikosi kuongeza. Kwanza mimi niko karibu sana na mbunga ya wanyama. Nikiwa kwangu nje ndovu nawaona wakiwa pale ng'ambo. Mimi nawaona nikiwa kwangu. Miaka mingi nilikuwa kazini nikifanya na kampuni ya Kenya Bus kule Nairobi. Shamba ile ambayo ninayo wakati huu niliipata mwaka wa sitini na moja nikiwa kazini vile vile.

Nikiwa kazini Nairobi, nilikuwa na bidii kabisa kabisa ya kuangalia ile shamba. Nilipanda minazi mingi kwa jumla lakini tukifika mwaka wa 1991 wanyama walivuka. Wakati huu kulikuwa hakuna waya ambayo ingeweza kuzuia. Walikuja wakavunja ile minazi yangu. Zaidi na zaidi wakavunja na kila kitu wakavunja na nilipostaafu mwaka wa 1992 nikawa na uoga wa kurudi kule shambani kwangu pale Kidongo, nikajaribu kupata shamba ingine kule Kibwezi, Makueni district. Nikiogopa, sasa nimeshatoka kazini nitarudi pale pale ambapo minazi yangu yote imeshavunjwa, nitakwenda kula nini na nishatoka kazini na ile pesa ambayo nimepewa na kampuni ndio ambayo ninaendelea na kusomesha watoto na kujisaidia na njia zingine. Lakini kwa bahati nzuri sasa kile ambacho nataka kifanywe wakati huu, ule waya ambao umeshawekwa juzi sasa uko chini umeshavunjwa na wale wanyama. Nimesharudi sasa, baada ya ule waya kuwekwa sawa sawa na wanyama wakawa hawawezi kuingia, nikarudi shambani kwangu na nikafanya kazi ya maana sana nikapanda minazi kwa wingi, ile midogo midogo sasa na ndizi kwa wingi. Sasa imeshavunjwa. Walishatembea kwangu siku hizi kuanzia January mpaka juzi wameshatembea kwangu karibu siku sita, na kila siku wakija nikiwa siko tayari na nikiwa siko karibu wanavunja. Katika katiba iliyoko sasa ambayo pengine itaendelea au haiendelei, kuna kifungu, sijui ni namba ngapi kwa sababu sijui kile kifungu lakini kiko, kinachosema ya kwamba mwanakenya atalindwa pamoja na mali yake, lakini naona kile kifungu ni kama kimesahaulika na ni kama hakifanyi kazi wakati huu.

Wanyama wanatembea vile wanavyotaka wakivunja vitu vya watu kama kwangu sasa. Mimi naonelea ile waya kwanza irudishwe, ndio, kwa sababu hatulipwi. Tukivunjiwa mali yetu, tulipwe, kwa sababu kifungu kinasema ya kwamba mwanakenya

atalindwa na mali yake. Sababu gani nisilipwe, na wale wanyama wakija kuangaliwa na wale watalii ambao wanakuja Kenya wanatoka pesa kwa wingi? Sababu gani mwananchi asilipwe akivunjiwa mali yake? Asante.

Ile waya ilikuwa na stima lakini stima ikawa ni kama inawachiliwa. Wakaja wanagusa wanaona hakuna kitu wanavunja, wanakanyanga tu, wanavunja, wanaruka, wanakuja, na wale askari hawaangalii. Hawako karibu; kwa hivyo ni kama wanyama ambao wanawekwa hivi hivi wawe wakitembea kila mahali bila mchungaji.

**Com. Swazuri:** Andika jina lako pale.

**Mr. Mutinda:** Nashukuru sana kwa nafasi hiyo. Mimi kwa majina ni Robert Mutinda Muia, mkaaji wa location ya Mwaluvanga, Kubo Division. Nikianzia pale mwanzo nitaanza kutaja utangulizi. Mapendekezo yangu katika utangulizi ni utaje, ama utangulizi ueleze hii katiba inamilikiwa na akina nani. Ya pili, itaje mwelekeo wetu wa kitaifa. Ya tatu, itaje mambo ama ieleze vipi taifa letu lilipopatikana, yaani ihusishe mwananchi. Ya nne, ionyeshe kuwa katiba hii mpya imetengenezwa na wananchi wenyewe. Iwe inaeleza wazi kuwa wananchi ni wenyewe, wanamiliki hii katiba kwa kuitengeneza wao wenyewe.

Mapendekezo yangu mengine ni katika upande wa uraia. Raia wa Kenya awe ni yule baba yake na mama yake ni wakaazi hapa, ni raia pia wa Kenya. Ya pili, uraia wa Kenya usipewe mtu mwingine isipokuwa yule baba yake ni raia wa Kenya. Hayo ni mapendekezo yangu katika upande wa raia. Nikiongezea pale, katiba ihakikishe kwamba hakuna ruhusa ya mtu kupewa uraia wa nchi mbili. Uwe ni uraia wa nchi moja tu pekee yake.

Naenda upande wa serikali na nimeandika memorandum yangu kubwa kwa hivyo nitaenda kwa ufupi fupi nikate kate kwa sababu ya muda. Mapendekezo yangu mwenzangu mmoja alikuwa ameyataja lakini nitataja halafu niongezee vile ambavyo ninaona ilivyo. Kuna hizi nguzo tatu za serikali ambazo ni bunge, serikali kuu na mahakama. Hizo nguzo tatu zinafaa kuwa ziko zimejisimamisha zenyewe; zinajitegemea, yaani ziko independent, na wakuu wa hizi nguzo wasiwe wakiteuliwa na mtu binafsi. Wawe wanateuliwa na bunge yenyewe ama bunge inashughulikia mambo hayo ya kujua ni nani anafaa kuwa Chief Justice na mambo kama yale. Huo wadhifa utolewe kwa rais, kwa ufupi.

Nitaenda katika upande wa bunge. Bunge lipewe wadhifa wa kuteua commission zote za kushughulikia mambo tofauti tofauti kama vile mishahara ya watumishi wa umma na hata pia bunge lipewe kuchagua ni wizara zipi ambazo zinafaa katika serikali yetu. Huo wadhifa usiwe ni wa mtu binafsi kuteua ni wizara ipi ambayo atapendekeza yeye mwenyewe. Bunge lishughulikie jambo hilo. Kuhusu wakuu ama maafisa wakuu wa kiserikali kama mawaziri na wakuu wa idara tofauti tofauti, pia mapendekezo yangu, ni bunge lipewe wadhifa huo ikishirikiana na kamati teule ya bunge.

Kuhusu wabunge maalum - mapendekezo yangu kuhusu wabunge maalum ni wateuliwe, si waondolewe. Wanafaa kuweko, lakini masharti ambayo ningependekeza yaweko, hawa wabunge maalum waweze kugawanywa katika wilaya zote. Kwa mfano

kila wilaya ikiwa wabunge ni kumi na wawili kama wakati huu kila wilaya ipewe number maalum ama idadi maalum ya kuteua wabunge maalum kulingana na vile utaratibu ulivyo katika mipangilio ya katiba mpya.

Nikiendelea pale nitataja kuhusu haki za kibinadamu na nitaingiza nyingi nyingi katika raia, dakika kidogo tu. Ardhi imilikiwe na mtu wa mwisho ambaye ni mtu binafsi. Apewe mamlaka ya kufanya chochote anachohitaji katika ardhi yake kuanzia chini kabisa mpaka juu kabisa. Ardhi iweze kurithiwa ama iwe katika sehemu fulani ambayo imetengwa ni ya familia nzima katiba ionyeshe kuwa title deed inaonyesha ardhi hii ni ya baba na mama na watoto. Ionyeshe inamilikiwa na watu watatu. Ya tatu kuwekwe kiwango maalum cha umilikaji wa ardhi. Mapendekezo yangu ni ardhi kila raia wa Kenya aweze kupata ardhi isipite hekari hamsini. Hiyo ni kumaanisha hata yule ana hekari ya zaidi hamsini katiba impatie hekari hamsini isiwe zaidi kwa sababu sote tunafaa kuwa sawasawa kama raia wa Kenya.

Ninamalizia. Katika vyama vya kisiasa, mapendekezo yangu ni kuwe na vyama vitatu tu vya kisiasa. Vyama hivi vihusike katika kuunda serikali. Iwe ni serikali ya mseto. Isiwe chama kimoja ndicho kinashughulikia jambo hilo. Na katika memorandum yangu inaelezea zaidi. Rais asiwe mbunge. Rais awe ni mtu amejisimamisha kabisa na katika mapendekezo yangu hata rais anaweza kuwa si wa chama fulani. Anaweza kuwa yuko independent. Amejisimamisha mwenyewe.

Nataka kumalizia kabisa. Nimeandika katika memorandum lakini kwa sababu umeuliza nitakujibu. Mapendekezo yangu, rais awe ni wa kiwango cha degree kwenda juu. Awe ni mtu wa miaka kuanzia ile katiba ambayo mwanzo imetaja thelathini na tano hadi sitini. Awe ni raia wa Kenya.

**Com. Swazuri:** Asante sana, tutasoma memorandum.

**Mr. Mutinda:** Nataka kumaliza mbili tu tafadhali. Namalizia basi, mapendezo yangu kura zikipigwa, sasa hiyo haitaingia kwa katiba sasa ni mapendekezo yangu. Uchaguzi mkuu nataka, kwa mapendekezo yangu, ufanywe baada ya katiba mpya kutoka hata ikiwa ni muda mngapi. Asanteni sana.

**Com. Swazuri:** Achia hapo na uandike. Thank you very much Bwana Robert, now we have Steve Kyalo na huyo atafuatiwa na Sammy Mutuku awe tayari. Haraka haraka kijana kuna watu wengi sana. Tupatie maoni yako ufuatiwe na Sammy Mutuku awe tayari.

**Mr. Kyalo:** Ningependa kuwasalimu, hamjambo? Mimi hii yangu ni document ambayo natarajia mtaisoma. Sina mengi ni hayo tu.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Sammy Mutuku. Hayuko. Suleiman Wandago atafuatiwa na Stanely Mwadime.

**Mr. Mutuku:** Hata mimi nafikiria yangu ni memorandum na nitapeana direct.

**Com. Swazuri:** Stanely Mwadime yuko.

**Mr. Mwadime:** Asante sana, mimi ni Stanely Mwadime na mambo yetu sisi tuliandika pamoja na Bwana Edward Mwanjole kwa hivyo sisi tunawajulisha tu pahali tunatoka halafu hii mapendekezo yetu tutapeleka kule. Sisi tunatoka Majimboni, katika Majimboni location. Box no. yetu ni 95, Shimba Hills. Kwa hivyo sisi mapendekezo yetu tumeandika basi tutapeleka kule mtakwenda kuyasoma.

**Com. Swazuri:** Kiruya S. King'oo.

**Mr. King'oo:** Asante sana commissioners, mimi naunga mkono mambo fulani halafu nitataja yale ninayosema. Kwanza nasema rais awe 35 years halafu awe ni mtu ambaye ana elimu ya kutosha kwa mfano kuanzia form four mpaka degree level lakini awe ni mtu mwenye hekima. Sio lazima sana awe ana degree. Iwe ni miaka hamsini. Pili, naona rais asiwe mbunge achaguliwe tu lakini asiwe mbunge kwa vile akiwa mbunge atapendelea sehemu yake. Sasa awe ni mtu ambaye si mbunge wa constituency fulani. Halafu nitaongea juu ya elimu, mambo ya education, kwa mfano tunataka watoto wapate elimu ya free kuanzia class one mpaka eight na iwe compulsory, na mzazi ambaye hatapeleka mtoto shule achukuliwe hatua za kisheria.

Pili, ningependa elimu ya computer iwe mandatory au compulsory, iwe ya lazima katika shule za upili zote. Hiyo inamaanisha ni lazima umeme ufike katika kila sehemu ambayo ina shule ya upili.

Tatu, huu mfumo wa Majimbo, kulingana na maoni yangu, unaweza ukaleta ukabila, tribal groupings na kingdoms ndogo ndogo halafu ukapotosha ule mwelekeo wa kitaifa. Lakini Majimbo ninayoyataka mimi ni yale ya kiuchumi. Kiuchumi vipi? Kinachopatikana katika jimbo fulani, percentage kubwa ibakie pale katika jimbo lile. Nataka asili mia sabini na tano itumike pale. Zile zingine ziende kwa serikali kuu.

Upigaji wa kura, kura zinapopigwa, yale mabox ya kupigia kura yawe transparent, yasiwe meusi. Wawe watu wanaweza kuona kura inaingia wapi, iwe hivi na kufanyike mchana. Mwisho, provincial administration. Mimi kulingana na maoni yangu, sielewi provincial administrators huwa haswa PC, ana kazi gani. Kwa sababu wale wanatakikana wawe replaced na provincial professional administrators. Unaona kama ni jambo la kilimo, kuna provincial agricultural officer. Kama ni jambo la security kuna provincial security officer. Hata district, division iwe hivyo hivyo. Wale watu wote ukiwatazama huwa wanafanya kazi moja tu kwa sababu kama ni swali la kilimo kuna mtu anahusikana na kilimo. PC huwa anafanya kazi gani?

**Com. Swazuri:** Kuna administration, sasa hawa kila mmoja ana kazi yake.

**Mr. King'oo:** Aah sidhani. Ile kazi anayofanya ya administration inaweza ikafanywa tu na wale watu wengine ambao wanashughulika tu na yale mambo. Halafu tukiteremka hivyo tuwe na chief ambaye atakuwa akifanya kazi zinazofanywa na DO at the moment. Akisaidiwa na sub-chief na chairman. Kuanzia DO kwenda juu mpaka PC pale nafikiria they are not serving any purpose. Kama ni swala la health tutauliza divisional health officer, district health officer, namna hiyo na yale mambo mengine. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante sana, andika jina lako pale. Sasa tuko na Uhuru Ndeto na atafuatiwa na Geoffrey Mwiyo.

**Mr. Ndeto:** Asante, mimi naitwa Uhuru Ndeto ni mkaaji wa Shimba Hills na ni mzee wa mtaa. Ya kwanza ni mashamba. Napendekeza mashamba kuna wazee wana mashamba na hawataki kukatia watoto mashamba hayo. Kwa hivyo kuwe kuna sheria inasema mzee kama hataki kukatia mtoto wake shamba achukuliwe hatua.

Pili, village chairmen wanafanya kazi kubwa sana kwa sababu DC akitangaza pesa kule anatangazia DO halafu DO anaambia chief, chief anaambia sub-chief, sub-chief anaambia wazee wa mtaa: endeni mkaokote pesa kadhaa huko mlete. Sisi wazee wa mtaa tunaingia huku na tunapambana na wananchi tunatukanwa, tunalete zile pesa. Lakini zingine tukiulizia hujui zinaenda wapi. Ukiulizia unaambiwa: wewe nenda ukusanye hizo pesa. Kwa hivyo wewe mzee wa mtaa ndiwe unatukanwa na wananchi. Michango ingine napendekeza iwe hakuna kwenda kuchangisha mwananchi. Kama pesa za sherehe nasikia kuna pesa za sherehe zinatakikana na DC, hizo ni zingine zinahusu wananchi. Mwananchi kule nyumbani sisi ndio tunatembea kule unakuta mwananchi amelala na njaa na hana kitu. Na mwananchi yule ambaye ameshiba ananyanyasa yule ambaye hana kitu. Kwa hivyo mtu kama sisi yetu, hizo pesa tunataka kujua kama kuna sheria imesema wakati wa sherehe wananchi wachangishe pesa za kufanya sherehe. Hiyo ni mapendekezo yangu. Sisi wazee wa mtaa maoni yangu nataka tulipwe hata kama sio kitu kikubwa tuwe kuna kitu. Kwa sababu unatembea kutoka asubuhi mpaka jioni na wewe una mtoto anasoma, huyo mtoto utamsomesha na nini, atakula nini? Na unahudumia wananchi na kazi nyingi wewe ndio unahudumia wale wanakaa tu kwa maofisi.

Lingine ni mashamba makubwa: Kuna watu wananunua mashamba, kama mbunge anakuja anachukua kama hii location ya Majimboni ananunua inakuwa yote ni yake na kuna mwananchi anateseka hana shamba, hana mahali pa kulima. Mapendekezo yangu ni mwananchi kama ni shamba awe na acre kama ishirini na tano mwisho. Mambo ya kuwa na acre kama mia moja hiyo nataka iondolewe kuwe na sheria ya kuwa hakuna. 25acres, ukizidi sana, hata kama wewe ni mbunge.

Haya, lingine la nne, ni mwalimu. Napendekeza, waalimu wanakaa mahali sana hata mpaka watoto wanaanza kuzoeana mpaka watoto wanataka kuwapa heshima, ndio unaona maovu mengine shuleni inatokea. Mwalimu akae katika shule miaka mitatu ikifika apigwe transfer apelekwe shule ingine. Lakini mambo ya kukaa sana mahali mpaka mtoto aanze Std. 1 mpaka 8, hiyo napendekeza iondolewe.

Ya tano, napendekeza mwananchi upande wa mbolea, serikali ambayo itakuwako au itatawala, isimamie bei ya mbolea, ya mbegu, mazao kwa sababu mwananchi anateseka kwa mambo ya mbolea na mbegu yule ambaye yuko chini hana uwezo na katika hapa Kenya wakati huu wananchi wale wengi ni wale wako chini hawajiwezi. Kwa hivyo, iwe inaangaliwa na serikali.

Ya mwisho, ni kuhusu ma-chief. Chief awe ndiye aliye na hukumu. Mambo ya DO, mambo ya PC, ya DC hatuoni kazi ambayo wanafanya. Kazi ni kukaa ofisini tu. Kwa hivyo na wazee wa mtaa wawe ndio wamepewa hiyo kazi. Na yangu ni hayo, asante.

**Com. Swazuri:** Asante sana.

**Mr. Simiyu:** Majina yangu ni Geoffrey Simiyu. Nitachangia kuhusu katiba ambayo ningependa kuiona katika nchi yangu ya Kenya. Nitaanza na elimu. Elimu iwe ni lazima kwa kila mwananchi wa Kenya kuanzia kwa mtoto mdogo mpaka wazee ambao wanaweza kusoma. Iwe katika katiba ya kwamba wanapata nafasi ya kujiendeleza katika masomo. Kwa swala la elimu pia, tumeona ya kwamba katika nchi hii tuna shida za kiuchumi na zinasababisha watoto wengine ambao ni werevu wakose kuendelea na masomo. Pendekezo langu ni kwamba katiba yetu iweze kuruhusu wizara ya elimu iandike ya kwamba mtoto yule ambaye anaweza kutoka shuleni aende akatafute kibarua afanye na baada ya mwaka mmoja au miwili aruhusiwe kurudi shule aendelee na masomo.

**Com. Swazuri: L**akini sheria inasema mtoto asifanye kazi mpaka afike miaka kumi na nane. Watoto kazi yao ni kusoma na kucheza.

**Mr. Simiyu:** Nimetumia neno mtoto kwa sababu ni msomi lakini iwe ya kwamba kama mtoto amefika secondary inawezekana kweli hajafika miaka kumi na nane lakini yuko secondary anaweza kuwa kama kidato cha pili na kuendelea. Kuwe na elimu kama ile iliyokuwa zamani mtoto anafanya KCSE Kenya Junior, anatumia hiyo certificate apate pesa arudi shule.

**Com. Swazuri:** Unataka mfumo wa zamani urudi?

**Mr. Simiyu:** Sio mfumo, naongea juu ya mtu mmoja ambaye ni mwanafunzi apate nafasi ya kuweza kuendelea na shule. Nasema hivi kwa sababu sisi mambo haya tuko nayo sasa mtoto akitoka shuleni itakuwa ni vigumu sana kwake kurudi shule mwaka mwingine miwili au mmoja baadaye. Nataka kusema kitu ambacho najua kinawezekana. Sitaki kusema tu kwa sababu nimepewa nafasi ya kusema. Okey, hiyo ni juu ya elimu. Point nyingine bado inahusika na elimu. Watu ambao wanapata kazi baada ya kufanya kidato cha form four maana wanaruhusiwa kisheria kufanya kazi na wangependa kuendelea au kujiendeleza kimasomo, napendekeza ya kwamba katiba yetu iweze kuwasiliana na wale employers ya kwamba wafanyi kazi waowanaweza kupewa nafasi ya kuendelea na masomo huku wakiwa bado wako kazini.

**Bishop Kariuki:** Question inaudible.

**Mr. Simiyu:** Ni sawa, hiyo imefanyika sana sana kwa wale watu ambao wako more qualified. Category ya juu sana kama watu waliofanya degree unakuta wanakuwa na nafasi ya kuendelea na masomo yao lakini wale watu wa chini nimesema form four kuendelea wale watu ambao hupata kazi ile tunaweza kuita ikiwa ni blue collar job hawapewi nafasi kuendelea na masomo.

Point nyingine sasa nikiwachana na elimu naenda katika uchumi. Napendekeza ya kwamba katika katiba ya Kenya, serikali iweze ku-encourage investors, these are multi-nationals, waweze ku-invest katika rural areas. Kwa sababu kitu ambacho najua kinapendeza watu ambao wanafanya investment ni availability of labour. Ninapendekeza ya kwamba watu hawa waje wa-invest in the rural area na serikali ikaweze kufanya infrastructure katika rural area kuwa conducive kwa hao watu ambao ni multi-nationals kuweza ku-invest.

Kwa mfano kwa wakati huu tunapata a lot of non-governmentals wanakuja huku kukusanya habari au kuelimisha umma na tunaona wanakuja na magari mazuri wako na allowances nzuri lakini wanakuja kwetu sisi raia tunapochangia tu hivi na waende hawaleti kitu ambacho kitatufaidi. Kwa hivyo kama serikali itaweza kuweka katika constitution uchumi wetu uwe decentralized sasa. Badala ya kusema kila kitu kifanyike Nairobi na Mombasa, uje katika rural areas where the farmer like in Shimba Hills yuko na machungwa na matunda kadhalika wa kadhalika. Walete industry za kuweza kufanya vitu kuhusiana na vile vitu vilivyo hapo kama mazao.

Naenda kwa point nyingine ambayo ni afya. Napendekeza ya kwamba afya iwe haki ya kila Mkenya. Na hapo ninamaanisha ya kuwa afya inamaanisha huyu mwananchi wa Kenya alindwe na sheria ya kwamba anaweza kupata matibabu anapokuwa mgonjwa isijalishe ya kwamba ana pesa au hana pesa, afya iwe ni haki yake. Afya kwa wamama- wamama tunajua ya kwamba wanafanya kazi nyingi sana katika rural areas. Kwa hivyo serikali ihakikishe ya kwamba mama anatunzwa pamoja na mtoto wake kisheria. Iwe ni sheria ya kwamba mama anaweza kupata matibabu kama vile vile sasa tunapata matibabu ya watoto bure wamama pia wapewe matibabu ya bure.

Point yangu nyingine ni katika hali ya kiuchumi. Napendekeza ya kwamba katika sheria ya Kenya kuwe ni kwamba mwananchi ambaye ni mkulima, maana Kenya watu wote karibu ni wakulima, iwe kwamba mkulima anapewa incentive ya kuweza kujisupport ku-produce mazao yale ambayo anayalima. Kukiwa ni kahawa, au machungwa, mwananchi wa Kenya apewe na serikali yake kitu cha kumsaidia kuweza kufikia point of production ya ile farm produce halafu serikali baadaye itaenda ku-deduct whatever it has put in it.

Administration:- ningependa kupendekeza ya kwamba iwe ni kitu ambacho kinaeleweka na raia. Yaani iwe friendly to the community. Kuanzia kwa wakuu, mimi sina shida na PC na whatever but we want administrators to be friendly to those people

he is administering ili kwamba wananchi wanaelewa ofisi yake ni ya kufanya kazi gani. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante sana.

**Mr. Ndalana:** Kwanza kwa commissioners nasema ni asante kwa nafasi hii ambayo nimepewa. Naitwa councillor Cyrus Ndalana. Kwa maoni ambayo sisi wananchi tunataka kutoa au kama mimi vile nataka kusema ile kitu muhimu sana kwa sheria, sheria ziko na sheria zinaendelea vizuri lakini sheria hazifuatwi. Kama ni sheria kama sasa kwa mfano watu hapa nimeunga mkono wamezungumza vizuri habari ya wanyama msitu, nini, kila kitu, lakini serikali mbele ilikuwa inasema kama mtu analiwa, au mimea yake inaharibiwa na wanyama analipa. Siku hizi hakuna kitu kama hiyo. Na KWS pia ilikuwa inasema italipa percentage kwa wakulima na wakulima hawapati hiyo kitu. Kwa hivyo inaonyesha serikali ina haja sana na wanyama kushinda wananchi na wananchi pia wana njaa sana hata pia hawawezi kununuliwa chakula wakapata nafuu au wakajisaidia.

Pili, sisi tunaona sheria kama hii ya mageuzi nini na nini, hiyo ni sheria lakini mwananchi yule aliye ndani ya taabu hafaidiki kwa hiyo sheria. Kama tuseme kwa mfano kwa shule kuna bursaries ambazo serikali inatoa inasema imetoa milioni hamsini, milioni fulani lakini hizo pesa zinaisha kabla hazijafikia shule zingine. Na sijui ni kwa nini haziwezi kugawanywa au sheria haiwezi kusema kila shule ipate ile haki ambayo serikali imesema kule.

Kuna hii ukulima:- tukianza kulima, sisi haswa hapa Shimba Hills, tuna mashamba yetu na tuna mazao mazuri na ni nchi nzuri na ni pahali serikali yaweza kufaidika, lakini tumekaa kama hatuko ndani ya sheria, hatuko ndani ya mzunguko wa ule wa kusaidiwa, maanake tuna machungwa na tuna kila kitu lakini hatufaidiki chochote. Serikali haiweki mikono kwa mwananchi ili imwinue apate nguvu ili aweze kuwa anaweza kujiendelesha. Upande wa kama korosho, machungwa.

**Com. Swazuri:** Unasema serikali isaidie kwa upande gani? Mikopo au barabara?

**Mr. Ndalana:** Mikopo ili watu waweze kujiweka au wacha mikopo pekee yake. Iwe ndani, kama ni kitu kinachoenda ng' ambo tuwe tuna uwezo kama ni machine ambayo iko pale hapatiwi iwe mikononi mwa wananchi, si iwe kuna mtu mwingine mwenyeji ambaye anasimamia. Mtu anachukua kama ni yake lakini ni kitu ya wananchi tunakatwa kila gunia ikienda inakatwa kitu. Ikienda kufika pahali unakuta mwananchi hakupata chochote. Iko chini kabisa na watu tuwe sisi tukiuza tunaweza kuuza direct hapana kuuza kwa huyu kwa huyu.

Ile ingine, sheria ni ngumu lakini ile muhimu kabisa sheria zinatengenezwa lakini hazifuatwi. Kuna ufukara ndani ndani mwa sheria na kuna watu wengine wanatumia sheria kama ni zao ama kama ziko kwao. Wana uwezo kushinda watu wengine. Unakuta mtu amepewa madaraka afanye kazi kama ni mtu wa serikali afanye hii afanye hii ndio unaona tunakosa kama ni ile nimesema bursaries tunakosa pahali pengine na kwingine kunapatikana. Kwa hivyo naona ile sheria kufuatwa ni sawa kabisa sheria si mbaya lakini kule kufuatwa kwa sheria ni kitu muhimu. Lengo langu liko hapo tu pekee yake. Kule sheria kufuatwa ni kitu sawa

sawa, na kama sisi tuko huko msituni tuna wanyama. Serikali inachukua mnyama kama kitu muhimu sana na inasahau kama imesema itatumikia. Tukipata uhuru tuliambiwa italinda mwananchi na kitu yake na kila kitu. Sasa huko watu wako msituni hata wale watu wakija KWS hawawezi kuja kuzunguka wakaangalia wananchi ni namna gani. Wamewacha sheria kando. Kwa hayo asante.

**Com. Swazuri:** Asante sana councilor andika jina lako pale na utusaidie sheria ifuatwe na wananchi. James Mainga na atafuatiwa na Zeinab Tchizuga.

**Mr. Mainga:** Mimi sehemu yangu ni Kidongo, sehemu ya wanyama. Nasema ni asante sana kwa katiba ya leo. Sasa pale kwetu karibu ndovu anatuvunjavunja na huyu ndovu amewekewa waya na ile waya akavunja ikawa ile waya kule haina moto. Sasa huyu ndovu aking'oa mnazi wangu ni ng'ombe, naweza kulipwa kama ng'ombe zile tunanunua Kinango, wapi vile tunanunua kama elfu kumi.

Jambo lingine Coast Province, tuna watoto wetu. Wakiingia Kwale siku ya kuandikisha watu katika kazi hao watoto wanaambiwa warudi Machakos ama Nairobi na wamezaliwa hapa hapa. Vitambulisho wanachukua hapa hapa Kwale na hiyo ni kitu kingine nacho kinatuweka hatujui tuko wapi. Warudi Machakos mahali mimi nimetoka huko na yule mtoto amezaliwa hapa hapa wakafanye kazi huko huko Machakos, ama wakaandikiwe Machakos. Si kazi hiyo inatokea Kwale ya army, polisi. Si tuna watoto wetu. Kuna kitu kingine kiko hapa Coast Province. Inaonekana hapa Coast inaitwa miji tisa. Hiyo miji tisa sasa si miji tisa ni miji kumi na moja kwa maana Wataita walikuwa bado kuingizwa Pwani ikawa sasa ni hawa Rabai na wale wengine hapa wadigo hivi sasa ikawa sisi tuko hapa unasikia saa ingine watu wanavurugana hapa shauri ya kuambiwa wabara kwao. Katika Kenya, mahali popote hata niko katika bahari huku ndani na ni Kenya siwezi kuambiwa niondoke kwa maana niko kwangu, niko Kenya. Nataka yule aliye katika Kenya akae Kenya asiambiwe kwenu ni wapi, ni Kenya. Asante sana.

**Com. Swazuri:** Asante. Zeinab.

**Mrs. Tchizuga:** Kwa jina naitwa Zeinab Tchizuga mwanakamati wa Matuga constituency, haya ndio maoni yangu. Kwanza kuhusu barabara - barabara zetu wale wanaohusika na utengenezaji wa barabara wanapokuja kwetu Kwale district na pesa watazitumia vibaya walazimishwe kuzilipa hizo pesa. Pili, serikali mfumo wa serikali tunaotaka. Tunataka Majimbo na Majimbo haya ni kumaanisha kabila lolote ambalo liko within Coast Province liwe litaishi pamoja na wenyeji kwa kuheshimiana na pia mapato yao yawe ya kuendeleza jimbo la pwani. Mapato yao kwa mfano kama wanafanya biashara yawe yale mapato yataendeleza jimbo la Pwani, sio kwamba wamekuja kuvuna na wanapeleka sehemu zingine.

Pia hapo nilikuwa nakuja. 85% ya mapato yanayopatikana katika uchumi wowote hiyo itabaki Coast Province. 15% iende central government. Hiyo ina-apply mpaka kwenye kazi. Kwa mfano Port au tourism industry, wale walioandikwa kuanzia ile top cream, 85% wawe ni wenyeji wa jimbo la Pwani, 15% ndio watoke nje ya jimbo la Pwani. Uchaguzi:- uchaguzi

tunaopendekeza sisi ni kwamba rais awe hata yeye anaweza kukabiliwa na sheria kwa hivyo tunasema tuwe na rais, kama ni mume, makamu wake awe ni mke. Tuwe na waziri mkuu na tuwe na governors ambao wataongoza haya Majimbo.

Wabunge wateuliwe kama vile ilivyo sasa. Umri wa rais uwe miaka arobaini na tano. Elimu yake iwe ni ya shahada. Mbunge ni miaka thelathini na tano. Elimu yake iwe ni kuanzia form four na kuendelea. Councillor elimu yake iwe ni form four na kuendelea na umri wake uwe ni thelathini na tano. Katika hivi viti tunaomba 40% viwe ni vya akina mama. Bungeni:- 10% iwe ni ya walemavu bungeni. Kwenye councils 20% iwe ni ya akina mama. 5% iwe ya walemavu. Katika wale wabunge maalum na ma-councillors maalum nafasi hizo zote zipewe akina mama.

Dini- dini zimekuwa nyingi kiwango cha kuwa imekuwa ni biashara. Kweli tunakubaliana na uhuru wa kuabudu lakini hizi dini zichunguzwe, zingine zimetuletea balaa ya devil worship.

Elimu:- tunahitaji vyuo vikuu katika jimbo letu. Tunahitaji colleges kama vile ya Utalii pia zipatikane katika jimbo letu. Shule za upili zile za kitaifa zipatikane katika jimbo letu na zile zilizoko zisaidiwe ili ziweze kujiimarisha ziwe katika kiwango cha kuweza kupatia watoto wetu elimu ya kisawa sawa. Elimu yenyewe, class cha kwanza mpaka cha nane iwe ni bure. Mzazi aachiwe majengo pekee yake. Vitabu na chaki, kalamu zote ziweze kutolewa na county council kwa sababu yale mapato tuliyoyatetea yatakuwa yanasimamiwa na county councils.

Pia hapo katika elimu kuwe na usawa mtoto wa kike na wa kiume na iwe ni lazima. Pia tunaomba katika uchaguzi wa commission tunaomba kwanza kuwe na commission maalum ambayo itasimamia mambo ya akina mama na watoto. Na commission hii ichaguliwe na bunge sio rais ili kupatikane usawa ambapo mfano mzuri tumeupata katika commission hii yetu ya mambo ya katiba kuna usawa kwa sababu kila jimbo limewakilishwa. Nafikiri nitakomea hapo kwa sasa. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Tumpate Kyengo Panga.

**Mr. Kyengo:** Mimi ndiye Kyengo Panga, kwetu ni hapa Mwapala. Matatizo yangu ni kama kusema hivi, juu ya skuli kubwa. Juu ya skuli kubwa kama vile ma-university yasiwe Nairobi pekee yake yawe mpaka hapa Mombasa. Ichaguliwe skuli zile za zamani, yawe university pale. Kama Krapf, ni ya kutoka 1864. Hiyo ni skuli ya zamani kabisa lakini serikali haikumbuki kuipa uwezo wa waalimu wa kutosha kuelimisha watoto. Tukitembea huko na huko watu wengi wanasema watu wa Pwani hawana elimu. Sasa elimu tutawezaje kuisoma na sisi hatuna skuli kubwa na hatuna nafasi ya kuondoka hapa kwenda Nairobi? Nairobi ni mbali, Nairobi kunataka mtu mwenye pesa.

Na nyingine, kwa upande wa silaha. Silaha zianatumika ovyo. Ukienda benki watu wanatumia mabastola, wanaibiwa. siku za nyuma haya mambo tulikuwa hatuyaoni sisi. Lakini utawala umekuwa mwAfrika silaha zinaua watu zaidi. hata kama huyo mkulima wafanya biashara yako utakuta vita tu, unyang’anywe pesa. Hizi silaha zatoka wapi? Na silaha zote hizi ziko mikononi

mwa rais. kwa hivyo pendekezo langu, ninataka silaha hizi zote zizuiliwe. Wananchi nao wanaweza kujiendeleza bila wasiwasi.

Neno jingine kwa upande wa machief. Kwa upande wa machief tunataka hapa pakiwa pana mduruma, chief awe mduruma asiwe kabila nyingine. Huwa hawezi kuelewa maendelezo mila za watu. Kuwe ikiwa ni mduruma awe mduruma. Ikiwa ni mdigo awe mdigo. Hivyo ndio naona inaweza kuwa sawa. Huyo mdigo si vile anavyoandika serikali. Vile anavyoandikisha kutoka zamani. Lakini hata ikiwa kuna mchanganyiko ile idadi kubwa ya wananchi ikiwa ni waDigo wawekwe chief mdigo. Ikiwa ni wakamba wawekwe mkamba. Neno jingine kwa mimi nafikiri nimemaliza.

**Com. Swazuri:** Haya, sasa nenda pale uandikishe jina lako. Mutinda, na kama hayuko tutasikiliza Donald Nyange. Karibu mzee Donald na atafuatiwa na Margaret.

**Mr. Nyange:** Mimi naitwa Donald Nyange mkaaji wa Shimba Hills. Mwanzo ningetaka kuchangia upande wa sheria. Tunaona katiba ya sasa inapendelea wenye pesa. Mtu kama mimi sheria hainichukulii vile inavyopasa. Kwa mfano tunasikia kuna mahakama za katiba. Sijui mtu kama mimi nitaisikia mwaka upi na nitajua nitapigia wapi? Kwa hivyo twataka sheria iwe sote tuwe sawa. Nionyeshe hatua za kufuata zile sheria nikianza hapa kama ni hakimu wa kwanza nikishindwa niende mbele wapi tuwe tuna maelezo ya kisheria.

La pili naomba mashule yawe bure. Tatu, pia ya kunyanyaswa kivyovyote vile tunataka kupungue. Kwa mfano naweza shikwa na askari nikazungushwazungushwa hapa mpaka hata kama ni kesho mambo bado sijui wapelekwa wapi na umefanyaje. Nataka sheria hizo askari watu waambiwe, nikishikwa nisimuliwe haswa niambiwe wazi. Maana umeshikwa kwa hivi na hivi na mwisho utafikishwa wapi. Kwa mfano si napelekwa sheriani au kama ni polisi station sasa nijue nikishikwa hapa naelekea polisi na kosa nimelijua ni lipi. Si kuwekwa mahali hivi pengine ulale mpaka kesho kama ni post ama ni wapi, sasa unajua utalala bila hata kula kitu. Utakataa wewe, una nguvu gani hebu sema? Mbele ya askari wa Kenya au wa nchi nyingine. Ndio nataka hayo katiba igeuzwe.

Upande wa shambani…

**Com. Baraza:** Unaona wao ndio wabaya ama hawajui kazi yao au hawana elimu kwa hiyo kazi yao au ni watu wabaya?

**Mr. Nyange:** Mimi naamini wana elimu na wamefundishwa. Mimi ndio nauita unyanyasaji, wanajua kazi yao, lakini sasa wananinyanyasa mimi maanake sijui chochote, nitababaishwababaishwa hapa mpaka nianze kutetemeka. Kama ningekuwa ninajua ningebishana naye lakini sina uwezo huo. Yaani anakunyanyasa kwa mfano sasa anishike hapa,

**Com. Baraza:** Halafu anauliza kitu kidogo.

**Mr. Nyange:** Si ndio kunyanyaswa huko? Halafu kuna mazao yetu shambani. tunaona hayo hakuna usawa katika vile yanavyoenda mpaka wewe uridhike kwa bei. Kwa mfano kuna watu wa katikati hapa. Kwa mfano kama tunauza biksa hapa Tiwi. Tuna korosho, tuna vitu vingi hata matunda. Sasa unajua utakapouza mtu akija kuyanunua hapa sasa au kama ni korosho zetu zinapelekwa pale. Bei hauwezi kujua wewe mwenye mali yako, hujui bei.

**Com. Baraza:** Na wewe mwenyewe ukisema nataka kupeleka korosho yangu kwa market kuna shida gani?

**Mr. Nyange:** Unazuiwa, kuna kitu ambacho kinakuzuia hujui. Sasa sijui imeundwa ni nani kama ni sheria. Hatuambiwi na wizara inayohusika au kama ni National Cereals Board haitwambii mali hii huku ina bei gani. Sasa kuna mtu atakuja hapa akwambie: mima nataka hizi korosho zako au hizi. Nafikiri nimemaliza.

**Com. Swazuri:** Margaret Odada.

**Mrs. Odada:** Mimi naitwa Margaret Odada kutoka Majimboni. Mimi nina maoni ya kwanza kabisa ni ya upande wa elimu. Rais wetu wa kwanza alisema elimu imekuwa ni ya bure kutoka class one up to class eight lakini kulingana na vile sasa kunaendelea inaonekana hakuna elimu ya bure. Utakuta mtoto ukimtuma shule anarejeshwa nyumbani saa nyingine. Wale wanaowarejesha nyumbani wanasema wanawatuma lakini ukiangalia ni kama mtu amefukuzwa. Utakuwa saa nyingine wewe hukuipangia pesa ya kupeleka shule lakini utakuta mtoto amerudi abruptly, itakubidi hata kama huna unga nyumbani ile pesa ya unga utatoa impeleke mtoto shule.

Kwa hivyo tunaumia sana na hii mambo kusema ile ukweli serikali ya Kenya wangechunguza na waangalie vile watasaidia wanyonge maana Mwenyezi Mungu hakutuumba sawa. Hatuko equal. Kila mtu aliumbwa na mapato yake. Kuna wale wanapata ya chini na kuna wale wanapata kidogo. Kwa hivyo ifanywe iwe ni free education, kwa wanyonge. Mimi naona ifanywe free education for all, maana sasa mimi nitasema sana upande wa elimu because I am learned and I know what education is. Utakuta mtoto wa mtu ambaye hajiwezi yuko very bright lakini mtoto anakaa nyumbani kwa sababu wazazi hawajiwezi.

Utakuta saa nyingine kuna kina mama wengine walifiliwa and they have their children, hawana pesa mtoto anarudi nyumbani na saa nyingine huyo ndiye huwa anaongoza classini. Sasa utakuta mtoto anakosa elimu kwa sababu ya pesa na wale waalimu wakuu wa primary hawataki kujua who are you. Wewe ni maskini na wewe ni tajiri. Hawataki kujua.

Ya pili mimi nilikuwa nasema kivyangu maoni yangu hata hawa waalimu na ma-headmasters wa hizi primary schools pia wangetolewa mbali kama hawa wa secondary ili akija pahali anaongoza hajui mtu yeyote ataanza kujua wale wako hapo saa ile ameletwa hapo, maana wale wako hapo inasemwa mtu ameletwa nyumbani. Sasa anaye meeting nyingine na wazazi wa mtoto sasa kwa vile ameletwa hapo analipisha. Kwa hivyo hata hawa pia wengine kama serikali ya Kenya wana uwezo watoe wengine hata kama ni bara, hawa wa huku nao wapelekwe huko ndio itaitwa Kenya imepata uhuru.

**Com. Swazuri:** Sawa endelea.

**Mrs. Odada:** Ya tatu, nitaongea kwa akina mama maana mimi ni mama. Nitasema juu ya ulevi. Ilisemwa pombe imepigwa marufuku, sio? Kulingana na vile ninasikia. Lakini inaonekana iliwachwa free, mtu anauza vile anataka. Kulingana na vile hiyo hali inaenda, inaonekana hakuna msaada wowote unaweza kusaidia watu maana wale wanaumia sana ni akina mama. Maana kuna waume wengine akienda hapo, si yeye ana elfu yake? Hatoki mpaka iishe hapo. Kule nyumbani mtotoamefukuzwa atakikana na vitabu, na vitabu, just one textbook, is 350 shillings na zinatakikana saa zingine seven of them. Where will you get that money? Sasa mimi nasema pombe ipigwe marufuku serikali ya Kenya na wasikubali hawa wanauza pombe polisi akienda hapo akipewa kitu kidogo anamwambia wewe endelea. Sasa akimwacha anaendelea yule anaumia ni mama.

**Com. Swazuri:** Sasa shida ni sheria, ama ni askari wanaovunja sheria? Kwa sababu sheria ya sasa imesema mnazi umepigwa marufuku.

**Mrs. Odada:** Mimi naona wengine wanavunja maana akipewa kitu kidogo hashughuliki na yule anauza hiyo pombe.

**Com. Swazuri:** Kama wewe ungekuwa Kinango jana ungeshtuliwa sana na watu kwa sababu watu wa Kinango wametuambia pombe ya mnazi ihalalishwe kwa sababu ni wengi wamesomeshwa na riziki kutoka kwa mnazi.

**Mrs. Odada:** Sasa mimi nitakuambia hivi, hata mimi ni mjaluo. Kwetu Kisumu tuna ma-professors ambao walisomeshwa na chang'aa lakini hiyo ina limit. Wajua something when it is too much it is not good. Si vibaya lakini iwe na limit yake maana if it is too much it is dangerous for some other people.

**Com. Baraza:** Kama Uganda wameweka saa za kufanya kazi na kila mtu halafu wanaenda kazi yao, wanapumzika kidogo halafu wanarudi kazini. Hiyo itakuwa ni sawa?

**Mrs. Odada:** For refreshment. Maana unajua kuna wengine wanaitumia for refreshment lakini kuna yule mwingine yeye anaiweka hiyo ndio chakula. Kule nyumbani wewe mama unabaki na watoto wanalia wana njaa, you must help mothers, Bwana. Yeye mwenyewe kwanza akija hapa aingia nyumbani anaupiga huo mlango na mguu anataka sima. Sima yote ameiacha kwa yule anauza pombe. For your kindness uandike.

Mambo nyingine, nimesikia mzee mwingine akisema hapa mambo ya university. Unajua hapa sisi tumekaa hapa Coast, tumekuwa watu wa Coast because we are Kenyans. Sasa tunapata taabu sana. School fees tunalipa, watoto wengine wamebarikiwa na Mwenyezi Mungu wanapita mtihani. Mtoto akipita mtihani unapata taabu. Saa nyingine amepita kwenda Nairobi University. Wewe mwenyewe hata hujui huko Nairobi. Hiyo university hujui ilijengwa wapi, Sasa mimi nilikuwa nasema

kwa maoni yangu, hapa Coast inajulikana sana ni pahali pakubwa ilete university na sisi tuwe na university yetu.

**Com. Swazuri:** Mama nitakuambia mimi ni mmoja wa wale ambao tuko katika area (inaudible)

**Mrs. Odada:** Sasa nilikuwa nauliza hivi, sijui kama ni vizuri nikiuliza? Kule bara imejengwa ma-university, huwa wanachanga pesa ndio inajengwa? Watujengee university huku. Wajua mtu akikataa kitu, hawezi kukaa bila sababu, ana sababu. Nyingine national schools. At least one to be in Coast Province maana kuna shule zingine naona kama Waa secondary naona ni ya kitambo sana, hata Matuga Girls is an old school, Kwale High imetoa watu wengi sana. Hakuna national school hata moja hapa Coast Province. Sasa, are we Kenyans kweli? It seems as if we are not Kenyans, wametusahau sana.

Jambo lingine, na nafikiri nitamalizia hapo. Haya mambo ya vyeo. Utakuta, chochote kikitoka Nairobi inateremshwa Kwale. Ikiteremshwa Kwale mara ndio district yetu, sasa utakuta kama ni ya akina mama, utasikia kuna mkutano siku fulani akina mama wanatakikana. Ukienda hapo kuna kitu iliteremshwa hapo wenyewe wamekula hata wamechoka sasa hata wakija huku unaona hawa wakubwa washachaguliwa tayari. Sisi wengine ambao tuko huku sasa tumekuwa reject. Hatujui chochote tunafanya kuletewa na wenzetu na ukiangalia unasema jamani kwa nini wanatufanya hivi. Hata sisi angaa tuchague watu wetu maana kama ni upande wa education we are also learned, we are not so much very primitive. Sasa mimi maoni yangu ni hii. Mambo ya mabunge na president nilikuwa nasema hivi. Wajua hapa kwetu wabunge wa kike ni uncounted. Tuna mmoja tu lakini tukienda kwa wenzetu they are uncounted lakini wako kule. Utakuta wako lakini hapa kwetu tuna wangapi wa kutoka Coast Province.

Sasa mimi nilikuwa nasema vitu vikigawanywa vigawanywe sawa na hata sisi akina mama wa huku, nafikiri sisi ndio hatujatoka nje. Kama kule kama inatakikana wawe tisa kwa parliament tuwe na hata kama ni wanne wa kutoka huku. Na mimi nafikiri nimemalizia hapo.

**Com. Swazuri:** Haya, Bwana Daniel Wambua na atafuatiwa na Ndei.

**Mr. Wambua:** "Ni kuseu". Ninayo mambo matatu ambayo nataka kuwakilisha kwa hii commission. Mimi ni mkaaji wa sehemu hii tu. Jina ni Daniel Wambua. Jambo la kwanza ni juu ya ukimwi. Shida hii ambayo iko juu ya ugonjwa naona imefika wakati wa sheria itengenezwe maana tumeambiwa na tumeambiwa ugonjwa hautaisha. Kwa hivyo kama imepitishwa ugonjwa ni wa kuishi na sisi naona serikali inayokuja tuitengenezee sheria yake. Kwanza ni kutengeneza mbinu za kusaidia wagonjwa wale ambao wanatayarishwa kufa. Wagonjwa ambao watakuwa na huu ugonjwa na wafanywe aje na waishi vipi na jamii yao watoto au mama na wafanywe aje, yaani kuwe kuna mpangilio.

Ya pili, juu ya hiyo sheria hiyo hiyo sehemu ingine yake ni kwamba wale ambao wataoana sheria iseme ni lazima wawe vetted, wachunguzwe, wale ambao wanataka kuoana ili hizi harusi zisichangie kusonga kwa huu ugonjwa. Shida itakuwa yule ambaye

atapatikana na ugonjwa atakosa bibi. Nafikiri ni sheria hiyo hiyo tu, basi wale ambao wana huu ugonjwa waoane ili wao wenyewe waendelee kukaa na wao waendelee na maisha na pengine katika hiyo shida ikiwa ni wagonjwa mtu akiwa ni mgonjwa naona sheria ipitishwe, wakatwe wawe hawawezi kuzaa maana utafiti unasema mtu akiwa mgonjwa akizaa mtoto si anakuwa mgonjwa pia? Sasa ni heri huyu mtu kama ni mwanamume awe castrated mwanamke afungwe kabisa awe tu anaendelea na miradi ya mwenzake lakini wasizae vitoto ambavyo vitakuja kufa baadaye. Hayo ni maoni yangu.

Swala lingine, ni gharama inayoletwa na wanyama wa pori. Mapendekezo yangu ni kwamba sheria ile tunayo ni kwamba mtu akiuawa na ndovu alipwe kiwango cha nasikia ni elfu thelathini, na mapendekezo yangu ni kwamba kiwango hichi kiinuliwe juu. Sehemu hizi zetu tunapozika mtu kwa heshima ni lazima tuwe na elfu sitini. Sasa ikiwa mtu ameuawa na huyu mnyama anapewa elfu thelathini hata mazishi haitoshi kwa hivyo ni maoni yangu kwamba jamii, yule ambaye ameuawa na mnyama wa pori inapodhibitishwa alipwe milioni moja. Sehemu ya pili ya hiyo ni kwamba, mtu akiumizwa na mnyama wa pori na pengine avunjwe alemazwe 60% ya mwili wake, alipwe nusu milioni, na akilemazwa kama 30% ya mwili wake, alipwe robo milioni.

Chini ya hiyo, kama tunapata shida nyingi sehemu hizo, ndovu waangushe minazi yetu kama mnazi mmoja ukidhibitishwa umeangushwa na mnyama, mkulima alipwe elfu kumi kwa mnazi mmoja. Mchungwa, mkulima alipwe elfu kumi pia. Acre ya mahindi mkulima alipwe elfu kumi na tano maana acre moja ya mahindi sehemu hizi zetu hutoka gunia kumi na sita za mahindi kwa hivyo alipwe elfu kumi na tano. Hiyo namalizia hapo.

Nataka nitoe ya mwisho ni urithi. Wewe kama una yako utaongeza kwa sababu hii ni ile nimefikiria. Ninaposema urithi nilikuwa nataka nisema urithi wa shamba na kwa sasa kama naishi shamba ya baba yangu ile sheria ambayo iko na title deed ni ya baba aidha baba anapokufa kugeuza hiyo title deed isome watoto wake. sheria iko complicated sana juu ya hiyo.

Inachukua muda mpaka kama ni mama tuwe naye aende kwa commissioner of oaths aende kortini, mambo marefu na ni jambo ambalo liko wazi. Kwa hivyo nasema ya kwamba kama urithi wa shamba ni kwamba mzee akishakufa sheria iwekwe wazi kwamba chief wa area na DO pengine wadhibitishe hiyo mara moja na mama na watoto wapewe title deed iwe converted kwa wao mara moja baada ya siku saba.

Mtu akifa tunatoa kibali azikwe saa hiyo hiyo. Basi pia mali yake, mama akiwa yuko hai pamoja na watoto iwe converted within seven days. Already ile nyingine nilikuwa nataka niseme ni kwamba wasichana ambao wako nyumbani na hawajaolewa, wasichana ambao wamezaliwa kwa mji fulani, kwa jamii fulani na bado hawajaolewa, kama atakaa pale na asiolewe kama siku hizi ilivyo, pia awe ni mmoja wa mriThi wa mali ya baba yao. Asante sana, nimeambiwa time yangu imeisha na mambo yangu ndio hayo. Thank you very much.

**Com. Swazuri:** Asante sana.

**Mr. Mutinda:** Kwanza ningependa kuwasalimia nyote, hamjambo? Tena kwa majina ni kama mlivyosikia, naitwa Mr. James Mutinda, from Shimba Hills. Niko na hoja kama nne ambazo ningependa kuongea. Ya kwanza kabisa ni kugusia kwa upande wa education, that is, elimu. Kwa kweli hii elimu ya kisasa inatoa kile ambacho tunakiita half baked professionals. Unapata mtu akiwa na miaka ishirini na miwili tayari yuko ofisini. Kwa kweli huyu ni mtoto kimwili, kiumri na hata kimawazo. Yale mambo ambayo anafanya ni yale ambayo amefundishwa tu pekee yake na ndio unaona hata miradi mingi ambayo inasimamiwa na hawa watu ambao wametoka kwa 8-4-4 are not successful, inaenda ikididimia. Hapo naona tungebadilisha hii 8-4-4 turudishe ile ya kitambo.

Pia ndio unaona hata migomo imezidi katika vyuo vikuu maana watoto wanaenda pale, they are given money by the government that, is through the loans, na wakifika pale hawajui pesa imetoka wapi na hawajui ugumu wa kutafuta hii pesa, so they have time to mess. Jambo la pili ni kuhusu humbi. Unakuta kwamba wazee wakisha-retire ama tukisha-retire tafadhali ningeomba mtu aki-retire wa serikali pia zile nafasi zake ambazo ameshikilia aweze kuziachilia vijana. Kuna vijana chipukizi ambao wametoka kwa hivi sasa ambao wanaweza kusimamia hizi nafasi tofauti. Unakuta mtu kama yeye alikuwa chairman ama alikuwa na cheo fulani katika kampuni fulani, akisha-retire unamkuta yeye bado yeye ndio amesimamia jambo fulani, ukienda huku bado ni yeye. Unakuta yeye pekee yake ana karibu vyeo kumi na kuna vijana ambao wako na the same experience na ambayo ni dot com, utaniruhusu kutumia hilo jina ambao wako na hiyo experience na wanaweza kufanya hiyo kazi kama yule mzee. Kwa hivyo yule mzee tafadhali aachiwe yale marupurupu yake ya uzeeni na hawa vijana wadogo wapewe hizo nafasi waweze kuendeleza nchi yetu.

Jambo la tatu ni kuhusu mazao. Mazao haya ni kama vile korosho, rangi na nazi ambazo zinatoka katika wilaya ya Coast. Ni vizuri kama kungekuwa na board ambazo kutakuwa zikitetea mazao haya. Tukiangalia upande wa Kericho kuna tea estate farms. Hizi farms ziko na boards zake na zile kilo ambazo mkulima anauza baada ya kila mwaka huwa wanapata bonus. Wakulima wa Coast sijui kama huwa wanapata bonus kutoka kwa rangi na hata ile bei wanayoambiwa inategemea na ni nani ananunua ama ni nani anauza wapi na lini. Kwa hivyo kama tungekuwa na hizi boards ingekuwa muhimu na hizi prices za hizi cash crops basi ichaguliwe na ile board but not the president.

Pia jambo la tatu ama la nne ni kuhusu budget. Wakati budget inasomwa, inasomwa in terms of nationwide. Ningeomba kama hii budget inaweza kutumiwa katika kila wilaya halafu pia ivunjwevunjwe ije katika kila district ndio tuweze kuona kama ni district gani ambayo haijajimudu kupitia upande wa economy. Tusiambiwe tu economy ni mbaya ama budget iko hivi na hivi when it is in terms of nationwide. Let us talk in terms of a district, tuongee kuhusu district fulani, province fulani halafu tukikusanya hiyo sasa ije in terms of nationwide.

Jambo la tano bado ningependa kuongea kuhusu ni hizi powers. Tunang’ang’ana kugeuza katiba. Kama tunataka tu-succeed, kwa maoni yangu, basi pasiwe na mtu yeyote ambaye is above the law. Maana tukigeuza katiba halafu kuwe bado kuna mtu ambaye yuko above the law that means ile katiba kwake yeye it is ineffective. Tuishi kama US mahali mtu akifanya kosa

anaambiwa bwana umefanya kosa. Tukichukua mfano wa Uganda, vice president wa Uganda ni mwanamke. Bwanake alifungwa na hakuweza kumtetea maana alikuwa amefanya makosa. Nafikiri sina mengi.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Bakari.

**Mr. Bakari:** Kwa majina naitwa Bakari. Nashukuru kwa nafasi hii. Nitazungumzia kuhusu kurekebisha katiba ambayo watu hawajui kile ambacho kinarekebishua. Katika Kenya ingekuwa kama (inaudible) itengenezwe katiba ambayo imeundwa kwa ajili ya watu. Jambo lingine ni kwamba hata ikiandikwa kiasi gani na hizi sheria watu hawajui hiyo itakuwa ni kazi ngumu kwa sababu watu wote katika Kenya hii wanazungumzia mambo ambayo kwamba yako katika katiba na hayako katika haki zao lakini hawaamini. Kama vile ambavyo (inaudible) kama ni mkulima apate kujua haki zake kutokana na hiyo area ambayo watu wameenda wakasoma kwa sheria ambazo ziko katika nchi hii.

Kwa hivyo katika katiba hii ambayo inatengenezwe ikiwa ni kifungu cha kuonyesha ya kwamba vile ambavyo angefanya na hakufanya. Kwa mfano ningeweza kutoa mfano mzuri katika nchi ni kama vile tulikuwa na problem ile ya titanium, there was a big uproar and outcry lakini it was only that the people were not shown what they should do and where the farmer should go and how he should do and it was a very simple thing. The farmer should have gone from A to B and then he takes up the matter but he's is being taken around. Kwa hivyo ningeomba kwamba watu waelimishwe kuhusiana na jambo hilo.

Jambo lile lingine, civic education. It should go back again to the people so that mwananchi yeyote wa Kenya akitoka kuingia kuwa mwananchi lazima awe na elimu ya kuelewa nchi yake na waziri ni nani kwa sababu hata leo ukaniuliza waziri wa elimu naweza naweza nisijue kwa sababu wanabadilishwa kila siku asubuhi na jioni lakini hawasomeshwi katika shule.

Next point ni kwamba katika mahojiano ambapo mama mtangulizi alikuwa ametoa kuhusiana na special interest ama special groups katika Kenya, mimi ningeonelea kwamba kama vile ambavyo inavyozungumziwa, wanawake wapewe nafasi sawa na haki zao. Kwani wamenyimwa haki zao na akina nani? Katiba ingetengenezwa ya kwamba ina haki za watu wote katika nchi hii. Isiwe ni mwanamke, isiwe ni mwanamume kwa sababu when we are talking of a woman and a man we are talking of two different people. Why should we not have a person? Katiba iwe ni ya kulinda wanaKenya. Mwanamke ni mwanakenya. There should be no special favour being made onto this. The law should be there for all to govern Kenyans and on equal basis na kama ni kwenda bunge bunge ama kama ni kuchaguliwa katika nyadhifa zote zile ambazo ziko wachaguliwe kulingana na nafasi zao na competition so that we may inherit a nation ambayo kwamba it is competitive, na sio watu kupewa kwa sababu nikiwa nitamchagua huyu mama kwa sababu kwamba pengine ni jirani yetu ama ni nani ama alichaguliwa kwa sababu ni rafiki wa chairman wa nani. Itakuwa haitatufaa, lakini achaguliwe kwa sababu ya uwezo na nafasi yake ile aliyo nayo na maarifa aliyo nayo. Hiyo naona kwamba ingefaa sana katika taifa iwe ni kitu ambacho kiwekwe maanani badala ya kutengeneza sheria ambazo zinasema wanawake wawekewe viti kumi na viwili vya nini. Waachiliwe ama wafundishwe wajue ni haki yao kupigania.

Wanawake katika Kenya ndio wengi kuliko waume, kwa hivyo kama ni kupeleka wanabunge wake wengi katika Kenya wanawake wangepeleka wabunge wengi katika Kenya, wakielimishwa haki zao na rights zao. Kwa hivyo hiyo ningeonelea ya kwamba, mama pengine it wont be, yageuze lakini ningeonelea ya kwamba hiyo ni muhimu kabisa kwa watu wote Kenya kuelimishwa na kupata kufahamu.

**Com. Baraza:** Sawa, hiyo ni maoni yako, lakini sheria inaongoza hii province imesema kwamba kumekuwa na inequality.

**Mr. Bakari:** Iondolewe iwekwe sheria ambayo inayosema….

**Com. Baraza:** Sheria ambayo inatuongoza kwa hii country inasema, kama hii nchi ya Kenya tumekuwa na inequality. Wanawake huamini kwa sababu hawana chochote, hawalipi mali wengine hata hawapelekwi shule sasa imesemwa tu. Tufanye namna gani ndio tuwainue kwa muda tu, wakipita kile kiwango cha kura wenyewe watakuwa able. Hiyo ndio sheria.

**Mr. Bakari:** Kwa hivyo maoni yangu ningependekeza katika katiba inayotengenezwa sasa, iwape watu wote kama vile ilivyo katika military hata katika America wakati ambapo kulikuwa na vita 1991, the women were in the front line where the men were because they are on the same basis and the same rights and whatever. So we should have a status whereby the Kenyans all should be equal and on the same identity. Kwa hivyo ningependelea, hayo ni maoni yangu kulingana na jambo hilo. Rais ningeomba kwamba viwe vipande viwili, yaani two terms, na iwe ya miaka minne na wala si mitano.

**Com. Baraza:** Na miaka awe na mingapi?

**Mr. Bakari:** Awe na miaka arobaini kuendelea. Na parliament should not be the supreme lawmaker alone kwa sababu kulingana na vile ambavyo wamefanya kama juzi kupitisha ya kwamba wajitakie mishahara ambayo inatia sisi kwenye shida. Imeonyesha lazima kuwa na counter check nyingine ambayo itatengenezwa kwa kuweza kuwazuia ama kuweza ku-check vile vitu ambavyo wao wanatengeneza. Kwa hivyo they should be quite a separate thing where if he passes a law also he should be checked by the executive to see whether it is practical.

**Com. Swazuri:** Asante sana.

**Mr. Macharia: S**ikitiko langu ni moja. Masikitiko yangu ni kusema, Mwenyezi Mungu aliumba binadamu kwa aina nyingi sana, tofauti tofauti, ndio akaweka alama ya vidole virefu na vifupi na ndivyo tulivyo. Masikitiko yangu ni kusema katika sisi waafrika na serikali yake iliyotoka nyuma na sasa tuliyonayo imeingia unyonge sana. Unyonge ni kusema, haswa mtu wa Pwani utajiri wake ni minazi na ndio inamwendelesha maisha yake yote. Leo serikali hii imeweka binadamu si kitu chochote. Ni mtu ambaye hana dhamani kuliko mnyama. Inaweka namna hiyo serikali yetu ambapo mtu wa Pwani kama tunavyosema kivuno chake ni minazi. Leo mnyama aitwaye ndovu yuala minazi na serikali haikumbuki mwafrika huyu. Ningetaka serikali iangalie

kwa upande wa binadamu amuweke mbele kuliko kumweka mnyama. Nikisema hivyo sisi hapa tunaliliwa minazi mingi sana na serikali inasema nilieni na limeni na mpande sana, walakini hakuna kulipwa. Je, hapo amesimama wapi serikali? Ni kuonyesha kwamba binadamu si chochote, si lolote ila mnyama ni kitu bora sana katika ulimwengu huu. Hapo naona masikitiko sana.

Mimi nazungumza. Nililiwa minazi mia moja na ishirini. Niko hapa Majimboni. Nilikuja kwa baraza hapa, ikawa mkuu wa wanyama ni nani, ni mtoto wa Ngala. Alikuja tamka mwenyewe hapa akasema hakuna kulipwa na ambapo zamani mtu alikuwa akilipwa. Nafikiri alizungumza hivyo kwa sababu kwamba ni mtu wa kiserikali lakini binadamu wengi waliudhika na msemo wake. Hapo tunaona kwamba kwa hakika ndio tunasema serikali inakumbuka mnyama kuliko binadamu. Ushafahamu? Kwa hivyo hayo ndio masikitiko yangu sana. Nikasema afadhali kwa leo niyazungumze na myachukue, maanake ni jambo la masikitiko sana.

Mnazi kuupanda unachukua miaka sita. Unaulea mpaka miaka sita ndio uanze kuzaa. Binadamu huyo huyo aulilie mpaka utakapozaa kisha uje uliwe na ndovu na asilipwe. Ni hasara ngapi hii? Asante.

Kwa hivyo kwa kusema, serikali yetu tunaipongeza sana. Unajua kuipongeza, hatusemi ya kwamba haiendi vibaya. Lakini mambo mengine huwa inakwenda kombo kombo. Serikali husema askari haina ruhusa kunyanyasa mwananchi lakini ukitembea huko ndani ndani kama town, hapa na pale wasimamishwa. Ukisimama wanakuambia, hebu toa kitambulisho. Ukimpa kitambulisho anakuchukua anakizuia. Anakuambia sina kazi. Anakuambia kazi wapi? Sina kazi. Anakuambia twende. Ukiandamana naye hapa na pale anakuambia toa chochote. Kwa nini, sina chochote, anakuambia utakwenda basi. Na tukaenda sisi tukaandika mambo mengine na utakwenda fungwa. Ukiangalia huna kosa lolote na anayekuambia hivyo ni ndugu yako ambaye ni mwafrika vile vile.

Mimi nimewahi kushikwa Mombasa. Naishi Mombasa mimi. Hapa nimekuja mwaka tisini hapa ni nchi yangu. Huo ndio mwendo wa polisi.

**Com. Swazuri:** Kwa hivyo tufanye nini kwa watu kama hawa?

**Mr. Macharia:** Watu kama hao kwa kisheria na awe anapatikana na hiyo, kazi yake ni kufutwa. Huwa hana haki ya kuwekwa. Kazi yake ni kufutwa.

**Com. Baraza:** Unataka mahali ambapo utaenda uripoti ya kwamba huyu polisi alinishika bila kosa au tutagundua namna gani? Unataka ofisi iwe hapa Kwale au hapa Shimba Hills ambayo wewe unaweza kwenda kuripoti kwamba huyu polisi amekushika.

**Mr. Macharia:** Polisi huyo huwezi ukamjua, kitu cha kwanza.

**Com. Baraza:** Nakuulizaje, utajua namna gani huyu polisi ni mbaya. Unataka hii katiba mpya iwe na ofisi ambayo wewe utaweza kwenda kuripoti ya kwamba wewe umenyanyaswa na polisi. Hiyo itakuwa ni sawa?

**Mr. Macharia:** Kama tamsha nasema ya kwamba kuwekwe ofisi ingekuwa sawa iwekwe ofisi, na wale polisi wanaofanya hivyo hawavai nguo za kipolisi, anavaa nguo za raia. Ukishaweka ofisi namna hiyo na kwenda kuripoti, wakati huo ukienda kuripoti utakuwa humjui namba yake. Si kila polisi ana namba yake? Sasa utamjuaje? Umenikamata wewe ni askari, tunaandamana hapa na pale, waniambia leta chochote, sina chochote, utakwenda mbele. Ukiandamana naye hatua ya hapa na pale pengine ni wawili watasema, wewe bwana tuko taabani tumuache. Sasa wachukua hatua kwenda kumshtaki, humjui namba yake.

**Com. Swazuri:** Nakuambia kwamba kuwe na pahali ambapo unaweza kushtaki hiyo ni hatua ya kwanza. Sasa jinsi ya kujua yule askari ni nani aliyemnyanyasa pia itachukuliwa.

**Mr. Macharia:** Hatokuambia jina wala hautajua namba yake.

**Com. Swazuri:** Ndio maanake nasema sasa itakuwa ni kazi yake kusikiza maoni yako na kujua huyo ni nani ambao askari hawaachiliwi hivi hivi. Kila mmoja hupewa sehemu yake. Kwa hivyo wale wanajua fulani leo yuko Majimboni, fulani yuko hapa. Sawa?

**Mr. Macharia:** Hiyo ni sawa.

**Com. Swazuri:** Florence.

**Florence:** Maoni yangu nataka katiba iwe ya kusaidia shida zetu kama sisi wakulima hatuna soko kuuza mali yetu ya shambani. Vingi vinaoza maana hatupati njia ya kupeleka vitu vyetu sokoni. Barabara zetu ni mbaya sana, hazifai. Wanaohusika hawafanyi kazi zao sawasawa maana hizo barabara hazingekuwa vile zilivyo. Wanyama nao wanatusumbua, ni wengi. Wanaoziangalia ama wanaoangalia mambo kama hayo naona kama hawatusaidii maana akina mama haswa wale ambao wameachwa na waume zao kama wamelima vitu vya kuweza kuuza hawana njia ya kuzipeleka.

Shida za shule, elimu yetu imekuwa na shida nyingi. Wazazi wameachiwa kila kitu mpaka ununulie mtoto kila kitu ndiposa aweze kuenda shuleni. Wazazi ni kama tumeshindwa na kuelimisha watoto wetu kwa sababu shida yetu kubwa hapa Shimba Hills ni wanyama na hizo barabara na mambo mengi hatuna soko ambayo tunaweza kuitegemea hata nikitoka nyumbani kwangu niseme naweza kuuza vitu vyangu na nikarudi nyumbani.

Hiyo ndio shida yetu kubwa, korosho zetu hazina bei, rangi haina bei, haya yote yametushinda kwa sababu tunakosa mahali pa kujitetea. Naomba wakati huu ambao tunaombwa maoni yetu ama tunaombwa kutengeza katiba tungelifikiriwa juu ya vitu vyetu maana havina mahali pa kwenda. Hata ukipeleka hutapata ile gharama yote uliyopata shambani haiwezi kurudi kwa sababu hatuna bei sawasawa, tunasumbuka.

**Com. Baraza:** Hiyo korosho ukienda kwa supermarket huko Nairobi kidogo tu namna hii ni shillingi mia. Hata mimi /.

**Florence:** Na hapa shambani basi tunanunuliwa debe nzima unapata karibu shillingi kama mia tatu na wewe umesumbuka kulimia, hatuna bei kabisa ni kama zinaenda bure.

**Com. Swazuri:** Asante sana mama. Nenda uandike jina lako pale. Elias Kimathi.

**Mr. Kimanthi:** Okey, ningependa kushukuru sana kwa wakati huu nikisema ya kwamba nawasalimu. Hamjambo? Kwa majina naitwa Elias Kimanthi na niko na points ambazo ningependelea kama zichukuliwe kwa umuhimu na zichukuliwe maanani kwa sababu hatungependelea kufanya jambo ambalo halina mwelekeo katika kumaliza hiki kikao. Jambo la kwanza ni kwamba kuna sehemu za point zangu zimegusiwa na wazazi wangu hapa. Ni kwamba mambo ya farm produce sitaweza kuongea zaidi kuhusu mambo yote, yashaongewa na wazazi wangu. Kuna mambo ambayo ningependa kuonelea ni afadhali yakiangaliwa katika sheria hii ya katiba nayo ni kuhusu umilikaji wa shamba na vijana wanapofika umri wa miaka kumi na nane.

Ingekuwa ni afadhali kijana akifika huo umri, anapewa sehemu yake mapema kwa sababu huyo kijana amekuwa ni mtu mzima na anaweza kupanga mambo yake ya utu uzima. Na katika sehemu ya kisomo, ningependelea ya kwamba kulingana na ile shida ya vijana wanaosoma mahali hapa, nimesikia kuna mpango wa university. Huo mpango ingekuwa ni afadhali kwa sababu kama watoto wetu, kama ni mapenzi ya Mungu, ningependelea haina haja kuelekea sehemu za bara kutafuta university wakitoka mahali ambapo ni karibu kama hapa. Kwa hivyo ningependelea university. Ingekuwa ni muhimu katika jawabu hili la kurahisisha haya mambo.

Kuna sehemu ingine ambayo ningependelea. Ikihusikana na hali ya kisomo, kuna vijana wengi ambao hawana uwezo wa kuendelea katika masomo yao. Kijana anapomaliza kama form four, huyo kijana amepita kwenda university na wazazi wake hawana uwezo wa kumgharimikia katika masomo yake zaidi. Sasa huyo kijana inabidi aende juu na chini kujishughulikia katika hali ya ku-raise pesa za kumwezesha kwenda university ama college. Ningeonelea kwamba huu mradi wa hali ya kutafuta mapeni katika kuendeleza masomo yake ingekuwa ni afadhali huyu kijana awe katika mradi ambao utakuwa umeanzishwa katika kijiji ambao ni mradi unaoweza kumpa huyu kijana shares ambazo zinaweza kumpatia mapato katika masomo yake.

Jambo ambalo huwa linanishangaza ni kwamba hapo ambapo nimefika huwa naweza kuona watu wengi wakishiriki katika mambo yale ya pre-wedding na watu wanahusika haswa kwa dhati katika huo mradi. Lakini kulingana na vile nimeona katika

hali ya kisomo, kama kijana ame-organise harambee yake ama mzazi, watu wanapuuza mambo kama hayo ya kisomo. Kwa hivyo ni afadhali jambo hilo litiliwe maanani sana katika sehemu ya kusaidiana ili kuangalia huo mradi wa masomo.

Halafu sasa ningeonelea huu mpango wa hii ofisi ya agriculture ingekuwa ni afadhali kama wangesaidia wakulima katika upande wa kuwasaidia na tusema fertilizer na seeds ambazo wangeweza kutosheleza mahitaji ya ambao hawana uwezo wa kununua mbolea, madawa hata na mbegu, ili wakati wanapoendelea kujishughulisha hivyo wanaweza kujitolea mhanga kuweza kuutumia wakati wao kushughulika katika mashamba yao.

Nikimalizia ni kusema ya kwamba wakati mbunge anapopewa mamlaka, huyo mbunge amejitolea sana katika mwanga kusimamia wananchi wenzake. Anaposimama katika bunge, anapopeleka shida za wananchi katika bunge, ningependelea ya kwamba wabunge wote wangechukulia huu mpango wakati anapo-raise issues katika bunge, yaani wamuunge mkono katika constituency yake. Hii ni kama wakati huyu mbunge anapotoa promises zake akiwa pale katika bunge, inafaa hizo promises kama amesema atahusikana na mambo ya barabara, atahusikana na mambo ya kisomo, atekeleze wajibu wake. Inapofika miaka mitatu na hajafanya lolote, basi huyu mbunge aangaliwe mambo yake na ang'olewe kwa kiti, na yule mbunge mwingine ambaye amejitolea katika mradi wa kuendeleza wananchi, katika miradi mbalimbali, aweze kupewa nafasi kwa sababu jambo ambalo tunataka kuangalia ni ku-excel bali si kurudi nyuma.

Na nikimalizia ni kwamba nashukuru sana kwa kikao hiki ambacho tumeanza kuanzia asubuhi kufikia sasa. Singependelea sana kusikia yote ambayo tumeweza kusema hapa yachukuliwe kama hayana maana sana, kwa sababu yote ambayo tunaongea hapa tungependelea yachukuliwe kwa dhati na yachukuliwe maanani kwa sababu manufaa ni kwa wananchi wote si eti tumesema jambo hapa na liende lichukuliwe hivi hivi ambapo……

**Bishop Njoroge:** Sababu tumekuja hapa ni kwa sababu hiki kikao kina maana kwa hivyo hayo unayoyasema hayasahauliki.

**Mr. Kimanthi:** Nashukuru. Kama mmekuja hapa basi huu mpango ningeonelea ni afadhali kabla election haijaanza hii katiba itoke ndio ile election itakayokuweko ifuate ile katiba ambayo imefanya tuwe tuko katika hiki kikao cha leo.

**Com. Swazuri:** Asante sana.

**Mr. Kioko:** Majina ni Wilfred Kioko. Maoni yangu ni machache na kwanza kabisa naanza na presidential powers. Zile presidential powers napendekeza zipunguzwe na ziwe shared between him and prime minister. Election of vice president - ninapendekeza vice president achaguliwe na wananchi kabisa kama president. Kusema hivi ni kusema president ama mtu anapojitokeza kusimama kama president awe na running mate ili tujue tukichagua fulani, mdogo wake atakuwa ni fulani au tuwe wananchi tunaweza kuja tukalinganisha tukaona hawa wawili wanaweza kutupeleka vizuri.

Ya tatu, constitutional appointments. Kuna baadhi ya ma-officer ambao nafasi zao ni constitutional appointment. Hizi napendekeza ziwe vetted. Wakati zinapofanywa na president, zipelekwe parliament ziwe vetted na zipitishwe. Hii itazuia president asije akachukuae watu wote kutoka kwa sehemu yake, pili, itamzuia kuchukua watu ambao ni wafisadi ambao hawatakuja kufanya vile inatakikana, au kuchukua watu ambao hawana zile qualifications zinazotakikana kwa hicho kiti.

Ile ingine ni education. Napendekeza primary education from Standard 1 to Standard 8 ifanywe free for all and compulsory. Iwe free and compulsory for everybody. Hii itatusaidia ikiwa katika vita vyetu ya kupigana na kutokujua.

Kuna infrastructure maintenance. Ninapendekeza hapa kwamba iwe ni criminal offence kwa yeyote ambaye anahitajika kutengeneza barabara akikosa kufanya. Ni apelekwe kotini na ashtakiwe with criminal negligence na kama ni mtu ambaye amepata gharama, amegharamika kwa kutofikisha mazao yake sokoni wakati unaofaa na iharibike, ni alipwe fidia.

Kile kingine ni ministries. The number of ministries should be determined and their numbers ziwe determined by parliament. Si mtu aamke asubuhi a-decide fulani nataka kum-appoint na aongeze ministries ili aongeze. I think fifteen ministries are enough. Ya mwisho, ni ku-devolve power from the central government to local authorities. Hiyo ninapendekeza ifanyike power ziwe entrusted with the local authorities.

**Com. Swazuri:** Question inaudible.

**Mr. Kioko:** Tunataka councilors wawe ni watu ambao wana elimu, tuseme up to form four. Zile powers za minister of local government na president ziondolewe awe hawezi kuja ku-dissolve our local authorities. Secondly, tunataka kwamba wale wafanyi kazi,chief officers wa local authorities wawe ni employees wa the local authority. That is to say they can be hired and fired by the local authority if they do not do what is expected of them. Thank you very much.

**Com. Swazuri:** Asante sana.

**Gloria:** Asante sana kwa nafasi hii ambayo mmenipatia. Zaidi ya yote niko hapa kushukuru ya kwamba mimi kama mwanaKenya ni mara yangu ya kwanza kuja kuelimishwa kuhusu sheria na mara nyingi wananchi wamekaa bila kujua sheria zao ndiposa mambo mengi yameenda kombo katika jamii zao ama katika maisha yao. Mimi langu ningeomba ya kwamba rais ambaye atachaguliwa kuongoza nchi yetu awe ni mtu ambaye anamcha Mungu na anamwogopa, ndipo ataweza kuongoza hata hiyo cabinet yake katika uongozi wa kumcha Mungu. Ningeonya serikali yetu kwamba isiweze kuruhusu ibada hizi zinazofanywa za mashetani kupewa nafasi katika nchi yetu.

Nchi iabudu Mungu mmoja na watu wawe na nafasi ya kushiriki katika kumjua Mungu na kumwogopa kwa sababu maongozi yote ya serikali yanatoka kwa Mungu na sisi sote tukimwabudu Mungu, tutakuwa nchi yetu itakuwa na amani na tutakuwa na

haki na usalama. Kunyanyasana kutaondoka katika nchi yetu. Ningependelea rais wetu awe na mamlaka hata kutembelea makanisa na kufundisha watu neno la Mungu ili wamche Mungu kwa sababu uovu unatokana na Ibilisi, na kama serikali yetu itaruhusu mashetani kuabudiwa tutakuwa tunapingana na Mungu wetu na yale tunayotaka kufanya hayataendelea. Yangu niliyokuwa nayo ni hayo na Bwana awabariki.

**Com. Swazuri:** Asante sana nenda uandike jina lako. Mama Mary Wambua, mbona mama una wasiwasi? Maoni yako tunayataka kwa vyovyote hata kama wewe ni nani.

**Mrs. Wambua:** Mimi sina wasiwasi. Kwa majina ni Mary na maoni yangu kulingana na katiba ama yale ambayo yametuleta hapa ni kwamba tukiangalia sehemu nyingi, ukiangalia katika sehemu hizi ambazo tuko hapa, ningependelea kwamba elimu kwa upande wa wasichana iimarishwe. Kwa sababu ukiona katika sehemu hii yetu ni kwamba kuna post ambazo zinaweza kuja na kwa sababu elimu imekuwa ya chini katika upande wa wanawake, unaona ya kwamba hakuna mwanamke ama msichana ambaye anaweza kuwekwa katika sehemu hizo.

Kwa hivyo ningependelea hasa sheria iwekwe kwa wale ambao wanaoza wasichana wakiwa wadogo, kwa sababu ukioza msichana akiwa mdogo ama ukioa msichana akiwa mdogo pengine huyo ni kiongozi angekuwa ni wa kesho ama angekuwa professor na unampotezea nafasi yake mapema. Kwa hivyo ningependa adabu iwekwe ya kifungo cha kiasi fulani. Wengine wanaolewa wakiwa wadogo na kunakuwa hakuna sheria ya kuwakinga. Iko? Kwa sababu unaweza ukaona mtoto amemaliza class ya sita ama ya saba na anapata mimba na anaenda na yule ambaye amechukua mimba na kunakuwa hakuna njia yoyote ambayo anaweza kujikinga.

Pia katika upande mwingine ningependa kuwe na sheria ya kwamba, katika ule urithi katika jamii tunaona ya kwamba wanawake ama wasichana ambao wamezaliwa katika jamii hawana nafasi ya urithi katika ile nyumba na kulingana na hali vile ilivyo ni kwamba mtoto wa kivulana na wa kisichana ni sawa kwa sababu zile kazi ambazo zinahitajika zinafanywa na wasichana na zinafanywa na wavulana na pia masomo huwa yako sawa. Kwa hivyo sioni njia yoyote ambayo itamfanya mtoto wa kisichana akose kupata at least chochote kutoka kwa wazazi wake. Either kwa shamba ama mali yoyote. Kwa hivyo ningependa kuwe kuna sheria ambayo inamkinga mtoto wa kike. Utaonelea katika sehemu zingine kwamba upande wa akina mama ambao wameolewa, katika sehemu hizi, utaona kwamba mama ambaye ameolewa hana nguvu pale nyumbani. Kwa mfano kama amekosana na mzee ama bwana, akishaambiwa aende kwao anachukua virago anaenda kwao na inakuwa hakuna njia yoyote ya kumsaidia. Ukiingilia kimila utaona ya kwamba pengine mila inamgandamiza lakini kukiwekwa sheria atakuwa ana mahali pa kwenda either kwa court ama mahali popote. Kwa hivyo ikiwekwa kama sheria nafikiri kutakuwa kuna njia ya kutumia ili na yeye ajipatie riziki yake kwa sababu kina mama ndio wanahusika haswa katika ulezi, watoto wa kiume pia katika watoto wa kike.

Nikimalizia, ni nafasi za kazi. Hiyo ningependekeza kwamba iwe nafasi za kazi ziwe ziko sawa bila kuchagua huyu ni nani ama

yule ni nani. Wavulana na wasichana. Pia kuangaliwe wasichana wapewe jukumu ya kufanya kazi zingine. Wasionekane kama pengine wasichana wa sehemu hii wameleghea ama hawana elimu ya juu sana pia na wao waangaliwe. Asante.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Nicodemus Musyoki yuko?

**Mr. Musyoki:** Basi kwa majina ni Nicodemus Musyoki. Nawasalimu nyote, hamjambo? Mimi points zangu nilizo nazo ni chache kidogo. Ya kwanza ni hii ya kuhusu kuabudu. Ama kwa kweli katiba yetu ya Kenya inaruhusu kuabudu lakini haijatilia maanani zaidi ama ika-clarify whom to worship. Ni kwamba tu tuwe na uhuru wa kuabudu na ndio maana tunakuta wakati huu tuko na shida. Makanisa yameanzishwa mengi hapa nchini na mengine yanashangaza. Unakuta mashirika mengine yanaungana, uabudu wao ni tofauti lakini kwa vile kuna uhuru wa kuabudu, hakuna sheria inaweza kuwafunga. Wakati huu tunalia huku juu na chini Mungiki, lakini hata hatujui wanaabudu nini na hata kama wanaabudu nini utawafanya nini na kuna uhuru wa kuabudu?

Kwa hivyo katiba yetu i-clarify, na hii mambo ya kusajili makanisa now and then, they should know why these people are coming to register new churches now and then. Kwa vile kama ni yale makanisa ya kawaida, Biblia kama ni ile ile, sijui ni kwa nini huyu mtu ana shida gani mpaka atoke kanisa hili na asonge kanisa lingine aanzishe yake pale kando. Kwa hivyo tuangalie kuhusu usajili wa makanisa ndio hii shida nyingi inaingilia pale.

Ile ingine ni kuhusu mayor hawa wa majiji ama wa manispaa. Wale jamaa ningependelea kama wangeweza kuchaguliwa na wananchi, hasa wakati wa uchaguzi pia kuwepo na nafasi ya kumchagua mayor, ndiposa tutakuta ya kwamba madiwani wale watakaoshinda basi kuna wale walikuwa wakipigania udiwani na kuna wengine walikuwa wakipigania both udiwani na u-mayor. Kwa hivyo mayor achaguliwe na wananchi kama wale wengine kawaida.

Pamoja, hii ya kuchaguliwa na wananchi pia, mwenyekiti wa kama county councils hawa wenye viti vya county councils, pia wanafaa wapiganie na wajitokeze kwa wananchi tuwaone, kwa vile wale ni huduma kwa wananchi, ni huduma kwa raia na basi kama mtu ataingia tu kule hata hatumjui, wengine hatujamwona lakini tuko naye.

Halafu kuna point ingine ya kuhusu fidia. Kwa mfano wakati watu wanaitwa kwa mikutano, unakuta kama mbunge, councillor ama hawa wakuu wakuu wa serikali ama wakuu wengine tu anawaambia nitakuwa mahali fulani, siku fulani kwa hivyo mningojee. Na mnangojea yule mtu mpaka jioni. Hatimaye unakuja kusikia kwamba, aah bahati mbaya tumepigiwa simu alipata safari ya America jana na hakutuma ripoti. Kwa hivyo ile siku tumepoteza, mbuzi zetu tumechinja, tumepika na hata wali mwingi pale tunaharibu chakula na wakati pia. Kwa hivyo mtu kama yule anafaa atulipe fidia wale ambao wote tumepoteza wakati ule. Kwa vile utakuta nchi kama America zilizoendelea ni kwamba hata kwa dating, you date somebody and you wont come, you have to pay that person. Kwa hivyo even in our country it should be the same.

Halafu kuna hii umilikaji wa ardhi, hiyo sitakuwa na shida sana kwa vile serikali yetu imetoa title deeds. Lakini sasa licha ya

kutoa hizo title deeds kuna shida pale pia. Minerals, wakati ukigunduliwa katika shamba lako kidogo kuna mahali kunatokeatokea kama oil hivi ama wakati umeita watu wa kukuchimbia kisima wakilipwa lipwa kidogo wanaona jiwe la dhahabu. My friend nakuambia ile sehemu is no longer yours. Yaani wakishapeleka ripoti mbele tu, kufikia pale kwa chief wajue kwamba pale kwako kumetokea dhahabu, bila shaka hiyo sehemu litakalokupata baadaye na itabidi ulitoe.

Ile sehemu hata ukija kuitishwa hauitishwi jinsi inavyostahili. Ni sawa, nikiachiwa ile dhahabu siwezi nikaifanya kitu ikiwa pale kwangu, lakini kwa nini wasije tu kwa njia inayofaa, bwana wewe wajua tumeona dhahabu hapa kwako, kwa hivyo tafadhali tungeomba kama utueleze wataka tukupatie nini ndipo uturuhusu tuchimbe hii dhahabu. Lakini utakuta wakati huu unafanya kuja kuambiwa tu sisi tunakupatia shillingi elfu mia tano na uondoke mahali hapa bwana. Ukikataa, utapoteza mia tano na utaenda zako. Kwa hivyo ningependa mambo yale yajadiliwe zaidi.

Ya mwisho ni kusisitizia kuhusu hii ya uchaguzi na katiba mpya. Mimi singependa kabisa uchaguzi ufanyike kabla ya kupata katiba mpya kwa vile kama tutapata uchaguzi kabla ya katiba mpya ni kwamba hii tume ambayo saa hii mpo imechaguliwa na mamlaka kutoka kule kwa rais na rais najua leo kulingana na katiba yetu kwamba akitaka anaweza kuivunja.

Kwa hivyo vile vile kama yule rais mwingine atachaguliwa kabla ya katiba mpya ataweza pia akiingia pale kwa vile hii katiba iliyoko ni nzuri sana kwa mamlaka ya rais. Sasa anaweza pia akafikiria akaona hiyo tume imeshindwa na kazi na ndio maana haikuweza kutayarisha katiba kabla ya uchaguzi mkuu, kwa hivyo naivunja na nitatengeneza tume ingine, na atakaa miaka mitano tena na hii katiba mpya. Kwa hivyo tafadhali ningesisitiza zaidi na wananchi wengine pia kwamba tusikubali uchanguzi kabla ya katiba mpya. Asanteni.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Sasa tutamsikiza Grace Ndunge.

**Mrs. Mwendwa:** Kwa jina ni kama mlivyosikia. Grace Ndunge Mwendwa. Kwanza nitazungumzia habari ya akina mama wakiwa maofisini. Utakuta kwamba kina mama wanapopewa majukumu ofisini kuna jambo hili linaitwa sexual harassment kutokana na wakubwa zao. Mimi langu ningeomba kwamba serikali itafute sheria fulani iweke kulinda hawa akina mama. Utakuta promotions zitakuja kutoka nje lakini sasa mama ambaye boss ameongea naye waende wafanye mapenzi na amekataa itakuwa na anagandamiza huyu mama na anamwonea hata inafika kiwango ya kuwa hawezi kumpa promotion kwa ajili ya kuwa amekataa maneno yake. Kwa hivyo yangu ni maombi ya kwamba kuwekwe sheria fulani kulinda akina mama kwa upande huo.

Ya pili, nitaongea kwa upande wa maternity leave. Unakuta akina mama nao wakati wako kazini na amefikia wakati wa maternity leave anapewa muda kidogo sana mpaka yule mtoto mchanga anayemwacha unakuta ni taabu. Kwa hivyo yangu maombi ni mama apewe maternity leave ya four months na ianze immediately akizaa. Hata kama atazidiwa pengine kabla ya wiki tatu hajazaa hiyo isihesabiwe lakini apewe ruhusa akapumzike.

Tunang'ang'ana sana na kupambana na huu ugonjwa hatari wa Ukimwi. Mimi ningeomba hili jambo la prostitution liangaliwe kindani sana. Na maoni yangu katika hili jambo ni kuwa prostitution iwe ni hatia. Halafu hawa akina mama ama pia hawa wazee wanaofanya hii kazi kama mtu hana otherwise pengine aangaliwe jambo fulani ambalo anaweza fanya ku-avoid hii prostitution ili watoto wanaozaliwa, hawana wazazi ama hii mambo ya kutupatupa watoto ambayo inalete results ya kuwa street children ipungue.

Halafu ya mwisho nitazungumzia pia habari ya street children. Yangu maombi ni kuwa serikali itafute mpango fulani hata kama ni kuanzisha fund fulani ya hawa watoto wale wanaweza kufundishwa yaani kuanzwe chuo fulani chao wapewe ujuzi fulani kama carpentry, kushona na mambo fulani. Kwa hivyo serikali itafute fund special ya street children ili kupunguza machokora. Ni hayo tu, asante.

**Com. Swazuri:** Na hawa machokora si wana wazazi?

**Mrs. Mwendwa:** Sasa kwa wazazi wa hawa chokora ambao wanajulikana, kama mzazi ana uwezo na anaweza kutunza huyu mtoto, na hataki kumtunza, basi achukuliwe hatua.

**Com. Swazuri:** Asante mama. Francis Marani.

**Mr. Marani:** Kwa majina naitwa Francis Marani. Sina mengi ya kuongea lakini nataka kuongezea kitu kimoja. Nataka hasa kuongea juu ya haya mambo ya bursary na mambo ya elimu yaani. Sasa tunapata kwamba kuna watoto wengi ambao wanafanya vizuri, they are bright, lakini wanashindwa kuendelea na masomo yao kwa sababu ya school fees. Halafu tena, serikali inatoa bursary na ina-benefit, hizo bursary wanatoa, watoto ambao wanajiweza ndio wanapatiwa hizo bursary. Wale ambao hawajiwezi wanakosa.

Kuna wale ambao wanatoka from the poor family na unawapata wako bright na wanakosa pesa ya kuendelea kusoma na huku serikali inaendelea kutoa bursary. Kwa hivyo nataka at least, wajaribu kuangalia haya mambo halafu wabadilishe ili bursary i-benefit wale ambao wako bright na from the poor family. Sina mengi ya kuongea.

**Com. Swazuri:** Musau Musila. Kuna yeyote mwingine ambaye hajatoa maoni na angelipenda kutoa maoni yake?

**Speaker:** Mimi nataka kuongeza.

**Com. Swazuri:** Kuna wengine wako bado halafu utakuja kuongeza. Musila, karibu.

**Mr. Musila:** Kwa majina mimi ni Simeon Musau Musila, na maoni yangu si mengi ni machache. Jambo la kwanza maoni yangu ni kuhusu uhuru wa kuabudu. Uhuru wa kuabudu nina maoni ya kwamba umekuwa mwingi kiasi ya kwamba watu wanashindwa waabudu nani. Kwa hivyo maoni yangu ni kwamba tumwabudu Mungu mmoja aliye hai na pia madhehebu yamezidi na hivyo ningeomba yapunguzwe ili tuweze kuwa na mwelekeo wa ibada.

Na upande mwingine ninaenda kwa upande wa kuondoa umaskini. Tumekuwa sasa hatuondoi, hakuna watu wanaondoa umaskini isipokuwa kupalilia. Umaskini unapalilia, unazaa, unazaa. Ni juzi tuliona watu maskini walio na vioski vya mboga vikivunjwa bila taarifa na bila huruma na watu hao wote ni maelfu nyingi, mpaka leo hawana namna ya kula. Sasa umaskini umezidi. Kwa hivyo ni maoni yangu kwamba hiyo hali ya kujimudu ya mtu wa kawaida iwe huru na kama ni kioski ya mboga, hata isiwe na leseni sababu kule anakotoa zile mboga na yale madawa yaliyopanda zile mboga tayari yalitozwa ushuru ukaingia mfukoni mwa serikali. Kwa hivyo huyo maskini asiye na namna, aachwe auze mboga yake,auze carrots zake kwa kiosk na asitozwe leseni.

Kwa upande wa kuondoa umaskini, ninaingilia kilimo. Mkulima amekuwa ni kama mpira ulio kiwanjani, unapigwa huku na kule, kwamba ananunua madawa ya kupandia kama vile mbolea, madawa ya kunyunyiza mimea inakuwa ni ghali pesa nyingi sana. Baada ya kuvuna yale mavuno inakuwa anaadhirika na zile bei kwa ajili ya kukosa masoko. Kwa hivyo nilikuwa na maoni kwamba wakulima ambao ndio wengi katika nchi yetu aweze kutambuliwa na njia za mauzo ziweze kutafutwa na zipanuliwe ili kwamba Kenya iweze kuwa na watu wanaojiweza.

Kwa hapo hapo kwa upande wa kilimo, tunaona zile pembe nazo zimeuzwa ni kama mtu anauzia adui wake sio ndugu yake. Zinakuwa ghali, kiasi ya kwamba mtu badala ya kupanua kilimo chake hawezi, maana kile kianzio, pesa za kuanzia hiyo kazi hana kwa ajili ya mazao kuwa bei duni na mazao kwa kukosa madawa yamekuwa duni. Kwa hivyo ni serikali ile itakayoshika usukani au itakayokuweko, macho yote yavuke kwa upande wa kilimo ili iweze kuboresha huyu mkulima. Na kwa hapa tulipo, tunajua biashara iko huru lakini tunashindwa tukiona ya kwamba mimea kama vile biksa imekuwa monopolized na mtu mmoja tu mhindi aliye na kiwanda cha biksa pale Tiwi.

Kwa hivyo hakuna mtu mwingine anayejitokeza kufanya biashara na huo mmea na anaamua akiwa huko huko, ile bei atakayonunua, imridhishe mkulima ni hiyo hiyo. Utafanya nini? Kwa hivyo, iwe huru huru kabisa. Isiwe eti kwa kuwa mkubwa ni mwenye kiwanda hawezi kuruhusiwa mtu mwingine kupata leseni ya kufanya biashara na huo mmea. Hivyo ni kugandamiza mkulima na umaskini kuzidi kuingia.

**Com. Swazuri:** Nakuuliza, mbali na kule, inauzwa wapi tena? Mkulima anaweza kuuza wapi?

**Mr. Marani:** Ni juzi tuliona watu wakinunua wana-export zinakwenda nje. Hatukufuatilia wanapeleka wapi. Lakini kwa ile competition ya ma-agent wana-compete na yule mhindi ilipanda mpaka mia na nne kwa kilo na walipoondoka,tulikuwa nayo

zamani hizo na mnyama aliyekula cooperative yetu ni yule aliyekula cooperative zote za Kenya, kwa hivyo ililiwa na huyo mnyama.

Kuna kifungu katika katiba ya zamani kinachosema eti raia alindwe na mali yake. Ni maoni yangu kwamba raia halindwi, anamalizwa. Kifungu hicho, kiangaliwe upya na kitekelezwe maana raia anataka ulinzi pamoja na mali yake na ikiwa hivyo usalama utakuweko na raia atafurahia. Kuna upande wa wanyama pori, zile area ambazo zina wanyama pori. Tunajua kuna wakati bunge ilikaa na ikaweka sheria kwamba raia akiuawa na mnyama pori asilipwe na ikaweka kitu kama kiini macho eti kama raia ameuawa alipwe elfu thelathini na hata hivyo, elfu thelathini hazifuatiliwi.

Haya, licha ya hiyo mnyama pori anaumiza raia. Akiumiza raia kama akifa hakuna mtu wa kumjali. Mnyama pori anakula mimea ya mkulima na akila ile mimea ni basi, hata yule mtu atabaki tu kuombaomba. Kwa hivyo ni maoni yangu kwamba mimi mwenye shamba, raia mwenye shamba kama mimi, yule anayeingia pale shamba, anaingia na kibali changu maanake wewe ukija utapiga hodi nitakuambia karibu. Sikukuambia karibu nimekuambia kwenda, huna budi utaenda. Kwa hivyo mnyama yeyote yule aliye pale shambani, yuko mikononi mwangu na vyovyote nitakavyomfanya nisiulize chochote. La sivyo tuifanye kwa upande mwingine. Amekula, ni mbuzi wako wewe serikali, huyo ni mbuzi wako, KWS nilete malalamiko uweze kunilipa kile changu kimeharibiwa na mbuzi wako. Ningependelea hayo maoni yawekwe mkazo sababu hiyo tumeona ya kwamba wanyama wa pori wametutawala na ndivyo wamekuwa na manufaa makubwa kwa serikali kuliko raia.

Kwa hayo nilikuwa nataka nifunge na oni kwamba maoni haya tunayaweka, yataandikwa yakuwe sheria zetu katiba yetu, nani atatekeleza? Nani atasimamia aone yanatimilika? Kwa mfano, kama mahakama imemshika mtoto wa mkubwa na yule mtoto hataadhibiwa sawa na mimi maskini. Yule mtoto itakuwa hivi hivi mpaka aondoke lakini maskini atabaki atalemewa na sheria mpaka ataadhibiwa. Sasa hii tofauti ya hawa wanadamu wanaKenya hawa, kimaoni yangu nataka iwe uniform, kibinadamu. Mtoto wa mkubwa au mkubwa na mimi mtu wa chini, uhai ni ule ule tulindwe na sheria moja.

Pia nashangaa kusikia ya kwamba wabunge wanajikatia mishahara na mimi nilikuwa na maoni kwamba isiwe kikundi cha watu au board au serikali inayojisimamia. Kama ni mishahara ya bunge, kuwe na commission fulani inashughulika na mambo ya bunge, kuongeza mishahara na marupurupu yao. Lakini sio wao kukaa waseme: okey, milioni tano eeh milioni kumi. Hiyo inakula pesa ya raia na sisi tunazidi kubaki maskini.

Kiserikali, mimi ningependa maoni yangu, kusiwe na serikali ya mgawanyiko kama Majimbo Majimbo. Tuwe na serikali moja kuu. Serikali moja kuu, iliyo na rais mmoja na mikoa inasimamiwa na ma-PC kama ilivyo, na ningependa kusema ya kwamba atambuliwe raia wa Kenya mahali popote alipo na awe na haki pale mahali, pasiwe na ubaguzi. Na kwa hayo machache ningependa kushukuru kwa ajili ya tume hii kunifikia, nilidhani sitaweza kuiona lakini iliahidi na imetenda. Asante.

**Com. Swazuri:** Asante sana, tutarudi tena na tukuonyeshe yale ambayo mmeandika kwamba mmeridhika nayo au la. Tutarudi

tena kwa miezi miwili. Tutaandika na turudi tuwaonyeshe, mliyosema ni haya. Je, mnasemaje? Mama.

**Mrs. Mwendwa:** Nashukuru sana Bwana Commissioner kwa kunipa nafasi hii. Nafikiri wakati nilikuwa nazungumza kuna kitu nimesahau inayoingiliana na hayo mambo ya ukahaba. Kuna mambo ya mavazi. Hakika mambo mengine wakati huu ni ya kusikitisha. Unaweza kutana na mama, ama msichana amevalia vibaya sana na hayo mavazi yake kutokana na vile anavaa ndiyo inafanya mambo ya kuvutia wanaume iweko. Kwa hivyo mimi ningeomba sheria iwekwe ya kupinga mavazi mabaya yasiweko katika wanaKenya.

Kama mama amevaa vibaya, wengine wanavaa nguo fupi mpaka hapa hivi unakuta ni kama yuko uchi anatembea nusu uchi. Kwa hivyo ningeomba sheria fulani iwekwe ya mavazi. Anayevalia vibaya ashikwe awekwe ndani.

Haya nikiongezea, kuna katika vijijini zetu kuna watu wanaitwa wazee wa mitaa, wanafanya kazi nyingi sana. wanasaidiana na administration katika mambo mengi sana. Na hao wazee wana miji na wana mafamilia yao na unakuta anatoka anazunguka asubuhi jua linakucha. Ili waangaliwe nao wasije wakaingiwa na ile tamaa ya kutaka kuchukua kitu kidogo kwa watu hivi, wangepewa hata kama ni kitu kidogo cha kujisaidia na kudumisha miji yao.

Mwisho, nitazungumzia habari ya Pwani kwa ujumla. Coast ni kama ambayo imesahaulika kidogo, hakuna university, hakuna national schools. Watoto wetu wakipita hapa mpaka waende national schools mbali na hali sisi wazazi wengine huku hatuna ule uwezo wa kupeleka watoto mbali sana. Unakuta mtoto atapita vizuri sana lakini ukihesabu ile gharama ya kupeleka mtoto national school ameitwa huko bara mbali, inabidi ushindwe. Kwa hivyo kungekuwa uwekwe kiwango fulani ya kuwa katika kila mkoa angalau kuwe na national school. Hata kama si mbili, kama moja na pengine hata university. Ni hayo tu.

**Com. Swazuri:** Unataka kina mama wote wavae (inaudible)

**Mrs. Mwendwa:** Hapana hakuna cha kulalamika. Hiyo ikiruhusiwa baadaye utakuta ¾ ama kila mtu ametembea uchi kwa vile imekuwa ni tradition. Hata wale watoto wanaozaliwa wataiga hiyo mfano, na generation inayokuja utakuta watu wanatembea uchi karibu wote. Kwa hivyo ingekuwa…….

**Com. Swazuri:** (inaudible)

**Mrs. Mwendwa:** Ndio hiyo pia nao wale wazee wa kitambo pia wangeendelea kufundisha mila lakini sasa ubaya ni vile wakati huu ni wakati mwingine wa dot com.

**Com. Swazuri:** Kuna mambo ambayo ni magumu kidogo ambapo vijana wa wakati huu wanavaa vile wanavyotaka na ndio inawaweka kwenye shida zaidi na ukikutwa unaambiwa sheria hii haikuruhusu. Damaris Mbaka.

**Mrs. Mbaka:** Kwa majina ni Damaris Mbaka na mimi ningependa kuchangia hasa kwa upande wa elimu na ningeonelea ya kwamba elimu hasa ya msingi ipeanwe bure katika nchi yetu. Na katika huo upande wa elimu kuna baadhi ya watoto ambao wanapata shida hasa ambao tuseme watoto ambao ni walemavu na hasa vipofu. Unakuta ya kwamba baada ya kuwa ameelimishwa ama amefundishwa pale Likoni, sasa itawapasa waende mpaka Thika. Kwa nini serikali isitusaidie sisi wananchi kujenga shule yetu ya upili hapa Pwani. Kwa hivyo ningeona ya kwamba watu ambao ni wa namna hiyo au walemavu kwa jumla watafutiwe mpango wa kujengewa shule yao.

**Com. Swazuri:** (inaudible)

**Mrs. Mbaka:** Lakini blind wanaenda Thika. Lingine ni kwamba ningeonelea ni vizuri sana kama kungewekwa sheria ambayo itamlazimisha mwananchi kama ataitwa kwa mkutano na akatae kuhudhuria ule mkutano kwa makusudi achukuliwe hatua, maana hakuna pengine popote ambapo mwananchi anaweza kupata elimu hasa kuhusu vile serikali inavyotaka. Kwa hivyo mtu wa namna hiyo achukuliwe hatua kiserikali.

Na la mwisho ni kwamba iwapo mwananchi yeyote yule ataepukana kiongozi awe ni wa kanisa au awe ni kiongozi wa aina gani, maana ukiangalia kwa wakati mwingi hasa viongozi wale ambao ni wanawake, wanadharauliwa sana na wanaume. Na mwanaume anaweza kusimama akamtukana yule mwanamke akamuuliza utanipeleka wapi wewe? Si wewe ni mwanamke? Kwa hivyo mimi ninaonelea ya kwamba ni vizuri sana kama kutawekwa sheria, mwanamume yeyote au mwananchi yeyote atakayemtukana kiongozi akiwa ni wa kanisa au kiongozi yeyote yule, yule mtu achukuliwe hatua. Na kwa hayo nasema ni asante.

**Com. Swazuri:** Asante sana. Mama Joyce Ngitu.

**Mrs. Ngitu:** Kwa majina naitwa Joyce Ngitu na maneno yangu ninazungumza ni mawili yale ambayo ninasikia inanigusa mwoyoni kuhusu matunda yetu. Matunda yetu hayana soko. Siku moja nilipeleka nikitarajia naweza kununulia watoto chakula. Kwenda sokoni nikakuta kwanza Tanzania imeleta inajaa mpaka mwisho. Soko hili linajaa mpaka mwisho, tuliokuwa na ma/ pale sokoni, nimewacha ile mali pale na kurudi sina chochote, huko Kongowea.

Sijui ni kwa nini mali zetu zinaingiliana na watu wa nje na sisi hatupeleki huko. Mimi naonelea ile soko tukiwaachia sisi watu wa Pwani tungekuwa ni kwa sababu tukipeleka sisi hatuna wengine wa kulete, tutakuwa tunapeleka tunanunuliwa. Sasa wale waTanzania walilete, sisi hatupati chochote pale. Wanaingilia kule kwa sababu bei ni nzuri na huko utapewa shillingi hamsini ama arobaini, ukipenda usipende ikalale na utamwaga. Hakuna njia nyingine. Yangu ya kusema ni hiyo. Sina nyingine ni hiyo soko na ukiangalia kuna nyingine, ukiangalia nazi leo tunauza bei mbili, sumni ndio pesa nyingi na ukiuza hiyo, mtoto atakula na atasoma? Naomba hizo soko zifungwe hizo za nje kwa sababu hata bata leo hatupeleki. Mafuta ni mengi. Tupeleke wapi? Utakuta ni

shillingi mbili. Nataka kiongozi apate kumjua Mungu.

**Mr. Willy Mutua:** Ikivunjwa na ndovu tulipwe elfu sita, shillingi elfu nne mbuzi kama ameliwa. Ingine nasema kama location hii ya Majimboni location tunataka ma-subchief wapunguzwe, kwa maana location hii ina ma-subchief sita. Ni ya nini, na zamani sub-chief mmoja amekuwa akitumika location tatu? Ninataka awe mmoja au wawili. Chief awe mmoja tu, asiondolewe.

Village chairman ndiye kila kitu, kwa maana chief mwenyewe anamtuma village chairman akafanye kukusanya pesa za wananchi. Kwa hivyo tunataka village chairman kwa maana ndiye kila kitu, apewe mshahara wa shillingi elfu saba (7,000) kwa maana yeye ndiye kila kitu. Hata sub-chief akifutwa kazi anatosha huyo. DO hapa hata hana kazi hapa. Tunataka DO aondoke hapa, tubaki sisi wenyewe. Nimemaliza. Thank you very much. Hiyo ni sehemu ambayo nimekuwa nimebakisha.

**Mr. Kimeu:** **M**imi napenda kutoa karatasi iliyoandikwa na wananchi wa Lukore kwa ajili ya…sitasoma, nitatoa.

**Mr. Wambua:** Mimi naitwa David Wambua Kioko. Mimi nitaongezea viongozi wote wawe wameoa. Kama ni wake wawe wameolewa. Pia siku ya uchaguzi iwe imewekwa wazi katika katiba. Pia serikali iweke loan ipatie vijana wale ambao hawana uwezo waanzishe biashara. Lingine, watu ambao wana mashamba makubwa walazimishwe kulima ama wapatie watu ambao wanaweza kulima kwa sababu ndio wanafuga wanyama wanasumbua watu. Ingine ya kuongezea, katika mazao yetu hatuna soko. Soko ambayo ni ya Kongowea kila siku mali inakuwa nyingi. Maoni yangu ingepangwa kila kama ni Shimba Hills, kama ni Kikoneni ipangwe siku yake magari kuingia kule, kwa sababu gari zote zikiingia kila siku mali ndio inakuwa nyingi. Kwa hivyo kila pahali papangwe siku yake kuingiza gari kule sokoni.

Ingine ya kuongezea ni mavazi. Wasichana wetu wamevaa mavazi ambayo hayana heshima ambapo miaka mingine ijayo wataenda kitupu, na ndio inaongezea mambo mabaya. Sina mengi.

**Com. Swazuri:** Mama, una point? Sema majina yako hapo.

**Mrs. Wambua:** Kwa majina naitwa Mary Wambua. Shida yangu ni kuhusu wanyama. Mimi nakaa kando ya forest. Haswa pale shambani silimi chochote, wanyama wamenisumbua, minazi yangu iliisha, michungwa, hata mahindi sasa sijapanda kwa sababu ya wale wanyama. Hata saa hizi nikitoka hapa, nafikiri nitakutana nao njiani. Sasa lazima nifanye haraka nisikutane nao. Kwetu ni kule mwisho forest pale mwisho kabisa. Tumepakana na waya kabisa. Aah mbali kabla ufike Kibambani. Huwa hamjafika, ooh huyu ni mgeni hajui. Tumepakana shamba hata maji twachota kwa waya kabisa.

**Com. Swazuri:** Kutoka hapa kufika nyumbani kwako ni umbali gani?

**Mrs. Wambua:** Mtamaliza masaa mawili. Eeh mtamaliza, mbali. Haya, shida nyingine ni kuhusu watoto wa shule pia. Tuna watoto ambao wamesoma, wamepita mitihani na wameketi nyumbani. Kwanza saa hizi niko na mtoto mmoja amemaliza shule,

mtihani, na hajaenda shule, shida ndio hiyo. Sina mengi, ni hayo tu.

**Mr. Elias Kimanthi:** Nami kwa jina ni Elias Kimanthi. Nilikuwa nishatoa point kule kwa hivyo nilikuwa nimesahau point mbili ambazo.

**Com. Baraza:** Mary njoo u-sign jina lako.

**Mr. Kimanthi:** Kuhusu huu mpango wa katiba. Hata mimi ni-mgeni katika huu mpango wa katiba ni kwamba sikuweza kujua kwa mapema katiba ni nini. Kwa hivyo ningeonelea ingekuwa ni afadhali katika hii katiba iwe inaweza kujulikana na kila mtu wakati hata kama kijana ameanza primary anajua maana ya katiba, kwa sababu hiyo katiba nadhania ndio iko na sheria zote, ili kitambo anapoendelea kukua anajua ile katiba yake ambayo inamtawala katika maisha yake. Ndio kila unajua kama mtoto anataka textbooks ni lazima aende kwa bookshop anunue textbook. Ingekuwa ni afadhali kama hii katiba ingekuwa authorized kama kwa textbook kila mtu akajua.

Halafu kuna mpango, yaani kuna hii tuseme kama mtu kijana akimaliza form four na ameenda college. Ile pesa ameharibu kwenda college yaani siwezi kusema ameharibu ametumia pesa nyingi kwenda college, na akienda college akimaliza kama ni diploma yake anaanza tena kama ni kuanza kutafuta kazi na huyu kijana ni maskini na huwezi ukam-compare huyu kijana na kijana wa tajiri. Huyu kijana ataenda na mabarua yake kwa maofisi anatafuta kazi na akienda akikutana na kijana wa tajiri, yule kijana wa maskini bado anaendelea kuhangaika kutafuta kazi. Kijana wa tajiri anachukuliwa anaingia kwa kazi, kijana yule ambaye wamefanya course pamoja, yeye anaendelea kutafuta kazi. Kwa hivyo hili jambo liwe ni kama tu ni usawa, ingekuwa ni afadhali. Na pia wakati huu kijana anaendelea kutafuta kazi, yeye amekuwa akitumia pesa nyingi college na huenda ikawa amemaliza hizo pesa na hana njia ingine ya kutafuta pesa. Anaenda kwa kazi, anaambiwa alete shillingi elfu kumi ndio aandikwe kazi. Hiyo itakuwa si picha mzuri. Kwa hivyo hiyo iwe kuwa wote wanaandikwa kazi, wanaandikwa na usawa na wakati unaofaa ili mtu akimaliza college anakuwa na target ile ambayo anasomea. Si eti anasoma, anaanza tena kiguu na njia kutafuta kazi. Kwa hivyo hayo ni mambo mawili ambayo ningependa kushukuru na nikimalizia kikao hiki ningependa niwapeane kwa Mwenyezi Mungu awabariki sana mnapoendelea katika huu mpango. Asante.

Meeting ended at 5.30. p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&**